





**Kinana** awashukia wanaokosoa cheo cha Samia

UKURASA 3

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa


# Nipashe JUMAPILI


MWANGA WA JAMII

Jumapili Agosti 14, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581037

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US

**NANDY, MWIJAKU WAPOTEZEANA**

UKURASA 20



# Kicheko bei za bidhaa kushuka

• **Serikali** yachukua hatua, mabingwa uchumi wataka bei gesi ya kupikia nayo...*Endelea ukurasa 2*

**HIZI NDIZO ZETU...**




Nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto akiwa ameiinua juu Ngao ya Jamii mara baada ya kuitwaa kwa kuifunga Simba mabao 2-1 jana katika uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

HOJA ZA CAG:

## Mifumo ya Bandari kufumuliwa

UKURASA 3

## Mbowe kufungua kesi kudai mali za mamilioni

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA: TULISEMA TUTAWACHAPA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Profesa Joyce Ndalichako, akizungumza katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani, Dar es Salaam juzi, na kuwataka vijana kujenga utamaduni wa kukopa pesa zinazotolewa na halmashauri na kurejesha mikopo kwa wakati ili waendelee kuaminika. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Bei za bidhaa kushuka

**Na Waandishi Wetu,** IRINGA

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema serikali itahakikisha bei za bidhaa mbalimbali nchini zinashuka ili kuleta unafuu wa maisha kwa wananchi.

Alitoa hadi hiyo jana alipozungumza na wananchi katika Jimbo la Isimani wakati akihitimisha ziara yake mkoani Iringa.

"Serikali ina dhamira njema kwa wananchi wake. Ninajua bidhaa mbalimbali zimepanda bei na tunaendeleza mapambano ili kuleta unafuu. Kama tulivyofanya kwenye ruzuku ya mbolea, tutafanya hivyo na kwingine," aliahidi.

Rais Samia alitoa ahadi hiyo baada ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, kuzungumzia kupanda kwa bei ya bidhaa, zikiwamo sabuni.

Waziri huyo alisema bidhaa hiyo imepanda kutokana na kupungua kwa malighafi ambazo hutumika kuitengeneza, kwa kiasi kikubwa zikiagizwa nje ya nchi.

"Ndugu zangu, serikali inatambua changamoto mnazokutana nazo kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali na hii ni kutokana na baadhi ya nchi tunazozitegemea kupata malighafi, kufunga mipaka yake. Hata hivyo, tayari tumefanya mazungumzo nao, tayari wamefungua mipaka," waziri huyo alisema.

Waziri Kijaji alisema kwa sasa tayari mipaka imefunguliwa na baada ya miezi miwili, bei ya sabuni itashuka.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema lengo la serikali ni kuhakikisha inaleta unafuu kwa wananchi licha ya mabadiliko mbalimbali yanayoikumba dunia kwa sasa.

Mbunge wa Isimani, Wiliam Lukuvi, aliipongeza serikali kwa kutoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo jimboni huko, akitolea mfano miradi ya umwagiliaji.

**ULINZI MAZINGIRA**

Katika hatua nyingine, Rais Samia amewataka Watanzania kulinda misitu kwa kuacha kukata miti ovyo kwa lengo la kupata kuni na mkaa.

Akiwa njiani kurejea Dodoma, Rais Samia alirejea ujumbe wake huo alioutoa mikoa ya Songwe, Mbeya, Iringa na Njombe, kwa wakazi wa Kata ya Mpunguzi jijini Dodoma aliposimama kuwasalimia.

"Kwenye suala la mkaa nilikuwa ninaangalia kutoka Mtera hadi hapa ni mkaa njia nzima, misitu inateketezwa lakini habari nzuri ni kwamba Wizara ya Madini inakwenda kuzindua mkaa unaoitwa mkaa rafiki unaotokana na vumbi la makaa ya mawe, jiandaeni badala ya kukaa porini kukata miti, mtachukua mkaa huu na kwenda kuuza kwenye maeneo yenu ili misitu yetu inusurike," aliagiza.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, aliwataka Watanzania kuendelea kutunza misitu na vyanzo vya maji ili kuzilinda rasilimali za taifa.

**■Imeandikwa na Francis Godwin na Martha Sambo (IRINGA) na Paul Mabeja (DODOMA).**

## Lori lilivyoziba barabara ya Moro-Dar kwa saa 7

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

ABIRIA wanaotumia barabara kuu ya Morogoro-Dar es Salaam, wamekwama kwa zaidi ya saa saba njiani baada ya lori lenye shehena ya magogo kushindwa kupanda mlima na kuziba njia, hivyo magari kushindwa kuvuka upande mmoja kwenda mwingine.

Akizungumza na Nipashe, mmoja wa abiria wa basi, Anicet Kiwale, alisema kuwa juzi alikuwa akitoka mkoani Mara na aliingia Morogoro Kituo cha Mabasi Msamvu majira ya saa nane usiku lakini hadi saa mbili asubuhi alikuwa bado hajavuka Mikese na foleni ilikuwa haisogei hadi askari walipofika kwa wingi muda huo na kuanza kusogeza magari.

Wasafiri wengine Salum Mrisho na Jackson Mahembe walioingia Morogoro kutoka Dar es Salaam kwa magari madogo, walisema walilazimika kutumia njia ya pembeni mwa reli ya kisasa ili kuepuka adha ya foleni walipopata taarifa kutokea ajali hiyo ya lori majira ya saa moja usiku juzi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fotunatus Musilim, alikiri lori hilo kufunga barabara usiku wa kuamkia jana na walichofanya ni kupata mashine ya kunyanyua shehena hiyo ya magogo na kusogeza gari kando ya barabara.

Alisema hatua zingine walizochukua kunusuru hali hiyo zinajumuisha kuruhusu magari kupita kwa awamu kwenye mwanya mdogo uliopo ili kupunguza foleni ndefu iliyokuwapo.

Kamanda huyo aliwasihi abiria na watumiaji wengine wa barabara kuendelea kuwa wavumilivu wakati shida hiyo ikiendelea kushughulikiwa ili magari yapite.

# Wachumi washauri bei ya gesi ishushwe nchini

**Na Beatrice Shayo**

WATAALAMU wa uchumi wameshauri kuangalia namna ya kupunguza gharama za gesi na umaskini kwa wananchi ili Watanzania wamudu ununuzi wa nishati hiyo na kuondokana na matumizi ya mkaa na kuni yanayoharibu mazingira.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti na Kupunguza Umaskini Tanzania (REPOA), Dk. Donald Mmari, katika mazungumzo na Nipashe jana, alisema bei ya mafuta inavyopanda na gharama za gesi zinapanda.

Alisema jambo la kufanya ni kuangalia namna ya kuwasaidia waagizaji wa gesi kwa kuwapunguzia gharama ili wananchi wamudu gharama zake.

Dk. Mmari alisema suala la kusaidia waagizaji gesi inayotokana na mafuta siyo jambo rahisi kwa kuwa linahitaji uchambuzi wa kina wa kitaalamu, akisisitiza huwezi kuweka ruzuku miaka yote.

"Huwezi kusema miaka yote unaweka ruzuku bila kujua hiyo fedha unaipata wapi kwa sababu unaweza kuharibu uchumi kwa kupunguza wigo wa serikali kutoa huduma nyingine, unaweza kujikuta unatumia kodi nyingine katika matumizi mengine unapotoa ruzuku, hapa lazima ujue unapunguza matumizi wapi na yana athari gani au unaongeza kodi wapi," alisema.

Mtaalamu wa Uchumi na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Abel Kinyondo, alisema gharama za gesi ni kubwa na hali ya uchumi wa Watanzania walio wengi ni mbaya na hata mkaa kwao wanaona ni gharama kubwa.

"Watanzania wengi hapa tunapoongea hata mkaa kwao ni gharama, kila wakati tunaambiwa tuachane na mkaa, twende katika gesi. Mkaa nao ni gharama, lazima tufahamu watu wetu tunaowaongoza wapo katika kipato cha chini,"alisema.

"Suala siyo kutaka au kutokutaka gesi, 'solution' (suluhisho) ya kudumu ni kupunguza umaskini kwa watu, hakuna mtu anayetaka macho yake yawe mekundu mpaka aonekane mchawi kwa kutumia kuni ama mkaa, kwa sababu hawezi gharama za gesi, anaona gesi siyo kipaumbele kwake," alisema.

Mchambuzi wa Masuala ya Uchumi, Profesa Haji Semboja, alisema kubadili matumizi kutoka nishati moja kwenda nyingine ni suala lisilokwepeka katika mifumo ya maendeleo na si kwa Tanzania pekee.

Alisema jambo hilo ni mchakato unaotakiwa kufuata mfumo, hivyo ni lazima kuwapo kwa sera ya kudhubutu, sheria na taratibu ambazo zinatakiwa kuwaambia wananchi nini wanachotakiwa kukifanya.

Prof. Semboja alisema bei ya nishati hiyo kwa Mtanzania kwa sasa haitofautiani na bei ya masoko ya kimataifa.

Alisema jambo lingine ambalo linaweza kutambulika katika soko ni kuangalia kodi zilizopo kwenye vifaa vya gesi katika mchakato mzima wa nishati, pia uwezekano wa kuzipunguza.

Alishauri maeneo ya mjini wanahitajika kubadilika kwa haraka kutoka matumizi ya mkaa kwenda matumizi ya gesi, akisitiza sheria imbane kila mtu kutunza mazingira.

HABARI KITAIFA

## Mbowe kufungua kesi kudai mali za mamilioni

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MWENYEKITI wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema kamwe hawezi kukiuza chama hicho, bali ataendelea na msimamo wake wa kupigania haki za Watanzania.

Vilevile amedai alishapokea vitisho vingi na hata kupewa fedha ili akiuze chama hicho na akapoteza mali zake nyingi za mamilioni ya shilingi, lakini hakufanya hivyo na ameendelea kusimama na wanachama wake na kwamba anajipanga kufungua kesi kudai mali zake hizo.

Mbowe alitoa kauli hiyo juzi mkoani Shinyanga alipozungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani ambayo yalifanyika mkoani hapa yakiratibiwa na Baraza la Vijana wa Chama hicho (BAVICHA) chini ya Mwenyekiti wake, John Pambalu.

Alisema baada ya kutoka Ikulu kuzungumza na Rais Samia na kuwa mkimya kwa muda, kuna maneno yalianza kuzungumzwa mtandaoni kuwa ukimya wake huo ulikuwa ishara kwamba tayari 'ameshalambishwa asali Ikulu', jambo ambalo alilikanusha vikali, akisisitiza hawezi kufanya hivyo.

"Ukimya wangu mara baada ya kutoka Ikulu kuzungumza na Rais Samia siyo kwamba nililambishwa asali, hapana! Watu wanapaswa kuelewa kwamba nimenyamaza kwa sababu kila jambo na wakati wake, mimi ningekuwa na njaa siku nyingi CHADEMA ningekuwa nimeipiga bei na kuhama nchi.

"Kama kuiuza CHADEMA kwa kulambishwa asali, ningekuwa nimeiuza kipindi cha nyuma ambapo nilikuwa nikipokea vitisho na kupoteza mali zangu za mamilioni, mimi siyo mtu wa njaa na sina tamaa, ninapenda vya halali," Mbowe alisisitiza.

Alisema licha ya kupoteza mali zake hizo wakati akipokea vitisho, muda ukifika atafungua kesi kudai haki zake, akisisitiza 'nikipewa sawa na nikikosa sawa', huku akibainisha kuwa kamwe hawezi kutawaliwa na mali, bali yeye ndiyo anaitawala mali.

Katika mkutano huo, Mbowe pia alizungumza suala la maridhiano ya kisiasa kati ya serikali, Chama Cha Mapinduzi (CCM) na CHADEMA ili kujenga misingi ya uhuru, demokrasia, haki na maendeleo bila ya ubaguzi wa kiitikadi.

Alitaja hoja tano za awali ambazo kwa sasa ndiyo wapo kwenye hayo maridhiano, kuwa suala la upatikanaji wa Katiba Mpya, serikali kufuta kesi zote za kisiasa na kusamehe vifungo kwa madai kuwa Uchaguzi Mkuu wa 2020 wanachama wa chama hicho wengi walibambikwa kesi, lakini akakiri kwamba kesi nyingi zimefutwa na kubaki nne.

Alitaja hoja ya tatu ni kurejesha mikutano ya hadhara kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa na kwa sasa wapo katika hatua nzuri.

Hoja nyingine ni kuhusu Halima Mdee na wenzake, lakini akasita kulizungumzia kwa kina suala hilo kwa kuwa liko mahakamani.

Kwa mujibu wa Mbowe, hoja ya tano ni kuwarudisha wakimbizi wa kisiasa ambao walikimbilia nje ya nchi na serikali iwahakikishie ulinzi ili wapate kurejea, jambo ambalo alisema liko katika hatua nzuri na watu hao wanakaribishwa kurejea nyumbani.

Alizungumzia pia hali ya vijana nchini, akisisitiza kuwa kuna mamilioni ya vijana kila siku wanazaliwa, lakini kasi yake haiendani na kasi ya ukuaji wa uchumi nchini, hivyo wengi wao kukabiliwa na tatizo la ukosefu wa ajira.

Mwenyekiti wa Baraza la Vijana Taifa (BAVICHA), John Pambalu, alisema tatizo kubwa ambalo bado linawakabili vijana wengi nchini ni ukosefu wa ajira na mitaji ya kuwawezesha kujiajiri wenyewe.



Wajasiliamali wakiwa wamepanga bidhaa zao katika kituo cha mabasi cha Mbezi mwisho jijini Dar es Salaam, japo Serikali imepiga marufuku kufanya biashara maeneo hayo. **PICHA: SABATO KASIKA**

HOJA ZA CAG

# Mifumo ya Bandari yaanza kufumuliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Bandari (TPA) imefanya upembuzi wa mifumo yake ili kushughulikia hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21 ya kuwa na mifumo inayosomana na hivyo kudhibiti upotevu wa mapato.

Vilevile, imebainisha kuwa kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Juni 2022, mapato ya TPA yameongezeka kutoka Sh. bilioni 910.4 mwaka uliopita hadi Sh. trilioni 1.095 mwaka 2021/22 huku ikitarajia kukusanya Sh. trilioni 1.224 kwa mwaka 2022/23.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Dk. Boniphace Nobeji, akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu mafanikio na mwelekeo wa mwaka 2022/23, alisema agizo la CAG ni kuwa na mifumo inayosomana ambapo wamefanya upembuzi ili kushughulikia hilo.

"Tunalifanyia kazi hilo na tumefanya upembuzi kuona namna gani mifumo kuiunganisha ili isomane na tuondoe kabisa karatasi na tujue kinachoingia sasa na wakati huo huo shilingi ngapi zimeingia na zilizotumika," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu huyo alisema ili kuhimili ushindani katika biashara ya bandari, TPA imeendelea kuboresha matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuondokana na mifumo ya zamani.

Alitaja mifumo inayotumika na inaendelea kuimarishwa kwa sasa ni mfumo katika shughuli za uhasibu, menejimenti ya rasilimali watu na utawala (ERP), mfumo wa kitaifa uliojengwa kuunganisha huduma za wadau wote wa huduma za bandari nchini (eSWS) ambao kwa sasa wanafikia 34.

"Kuna mfumo unaounganisha huduma za utekelezaji (meli na shehena) na malipo ya huduma zote kielektroniki katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara (TOS), pia mfumo wa POAS ambao unaunganisha huduma za utekelezaji na malipo ya huduma zote kielektroniki katika Bandari za Maziwa Makuu na eneo linalohudumia meli ndogo na majahazi - Bandari ya Dar es Salaam," alisema.

Alisema kuna mfumo jumuishi unaowawezesha wadau wengine kama mawakala wa forodha kufanya malipo kwa njia za kimtandao (TePP).

Kuhusu mifumo ya ulinzi na usalama, alisema TPA imefunga mifumo ya kisasa ya kiulinzi na midaki ya kisasa (scanners) kwa ajili ya ukaguzi wa mizigo ya wateja ambayo imeunganishwa na mifumo ya kisasa inayosomana na bandari zote katika ofisi za TPA Makao Makuu hadi wizarani. Dk. Nobeji ambaye pia ni Mkurugenzi wa Mipango, Ubora na Udhibiti Vihatarishi wa Mamlaka hiyo, alisema TPA imejipanga pia kuboresha mifumo wa reli ndani ya Bandari ya Dar es Salaam.

"Mradi huu upo katika hatua za ununuzi wa mkandarasi na ukikamilika, unatarajiwa kuongeza ufanisi wa Bandari ya Dar es salaam kwa kuwa itaongeza kasi ya uondoshaji shehena ndani ya bandari," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu huyo pia alisema TPA ilifanya tathmini ya bandari zisizo rasmi ambapo hadi sasa zimerasmishwa 20 kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Pamoja na hayo, alisema Bandari ya Mwanza imeanza kuhudumia shehena ya makaa ya mawe kwenda Uganda na hadi kufikia Julai mwaka huu, tani 4,514 za shehena ya makaa ya mawe zimesafirishwa kwenda katika nchi hiyo.

# Kinana awashukia wanaokosoa cheo cha Samia Ikulu

**Na Waandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kanali mstaafu Abdulrahman Kinana, amewashukia wanaosema Rais Samia Suluhu Hassan ni Rais wa Katiba, akisisitiza kiongozi huyo alipatikana kwa mchakato uliotokana na uchaguzi.

Kinana alitoa kauli hiyo jana wakati akihutubia katika Kongamano la Kumpongeza Rais Samia kwa kasi nzuri ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi wa CCM ya mwaka 2020-2025 lililofanyika Mkoa wa Kaskazini Unguja, akikumbusha kuwa alipata nafasi hiyo kwa kuchaguliwa na kwa mwongozo wa katiba.

"Tangu Rais achukue uongozi kwenye taifa letu, kuna kauli nimekuwa nikiisikia kwamba Rais Samia ni Rais wa Katiba, kila chama kinapomchagua mgombea mwenza kinafuata vigezo, hivyo alipimwa na akaonekana kuwa anaweza na anamudu kazi hiyo na ana utaratibu mzuri wa kuongoza nchi, anafanya kazi nzuri na tunampongeza.

"Wanaosema Rais ni wa Katiba, hajachaguliwa siyo kweli, Rais anapopigiwa kura na makamu wake na yeye ni vivyo hivyo, hivyo Rais Samia alikutana na mchakato wa uchaguzi, wale wanaosema Rais wa Katiba msiwasikilize, wana ajenda yao," alisema.

Kinana aliongeza kuwa Katiba inasema kila chama kitateua mgombea na mwenza, na kwamba wote wanapatikana kwa matakwa ya katiba na siyo ya watu.

Alisema kuwa kwa kipindi ambacho Rais Samia amekuwa madarakani, amefanya mambo makubwa na wanampongeza kwa kazi anayofanya.

Alibainisha kuwa kazi haiwezi kufanyika bila fedha, hivyo Rais Samia anajituma kuzitafuta ili kuleta maendeleo na ameweka utaratibu mzuri wa ukusanyaji kodi na kutafuta fedha za misaada na kwamba katika hilo anakubalika na anajua namna ya kuzungumza na wafadhili.

Pia alisema ni lazima waombe fedha za misaada, mikopo na kuwaleta wawekezaji kuja kuwekeza nchini ili kukuza uchumi na kuongeza ajira, akisisitiza kuwa kila kutakapokuwa na uwekezaji mkubwa nchini, kutakuwa na kipato kikubwa kwa serikali na ajira kuongezeka kwa wananchi.

Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM, Shaka Hamdu Shaka, alisema chama hicho kinaongozwa kwa msingi ya Katiba na kanuni, akisisitiza kwa utaratibu wa chama hicho, Rais Samia na Dk. Hussein Ali Mwinyi wa Zanzibar watamalizana nao 2030 na kama kuna mtu ana ndoto, aziweke pembeni.

"Ninataka niwahakikishie tulipotoka pazuri, tulipo pazuri zaidi na matarajio ni makubwa kwa Rais Samia na Dk. Hussein, wanafanya kazi nzuri na hiyo ndiyo tuliyowatuma ya kuwaletea maendeleo Watanzania.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alitaja mafanikio mbalimbali waliyoyapata katika mkoa huo chini ya uongozi wa Rais Samia na Dk. Mwinyi, ikiwamo ujenzi wa bandari, madarasa, barabara na ununuzi wa boti kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za maendeleo.

*Imeandaliwa na Maulid Mmbaga, Beatrice Shayo na Rahma Suleiman

# TRA yaanika mikakati ya kukusanya tril. 24/-

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Mapato (TRA) katika kufikisha lengo la makusanyo iliyopangiwa ya Sh. trilioni 23.65 kwa mwaka wa fedha 2022/23, imejipanga kufanya mambo saba ikiwamo kukabiliana na vishoka na matapeli wanaoichafua na kusababisha upotevu wa mapato au kushindwa kuyakusanya kwa wakati.

Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi, Richard Kayombo, alibainisha mikakati hiyo juzi jijini Dar es Salaam alipozungumza mipango yao kwa mwaka huu wa fedha na mambo waliyofanya.

Kayombo alitaja jambo la pili ni kuongeza usimamizi wa utoaji wa risiti kwa njia ya EFD pamoja na kuziba mianya ya udanganyifu mbalimbali.

"Tatu, tutaongeza usimamizi wa utoaji wa risiti kwa njia ya EFD pamoja na kuziba mianya ya udanganyifu mbalimbali. Pia tutaimarisha mifumo iliyopo pamoja na kuzindua mifumo mipya ya kukusanya kodi mbalimbali ili kuongeza ufanisi, urahisi wa ulipaji na ukusanyaji na kuokoa muda na gharama kwa mlipakodi na TRA,"

Kayombo alitaja jambo la nne ni kuendeleza maandalizi ya Bahati Nasibu Kubwa ya EFD baada ya kukamilika kwa majaribio ya sasa yanayondelea Mkoa wa Kikodi Tegeta ili kuhamasisha utoaji na kudai risiti za EFD.

"Tano, kuongeza kasi ya utoaji elimu ya kodi kwa makundi mbalimbali pamoja kuhamsisha ulipaji wa kodi kwa njia za ubunifu na shirikishi ikiwamo Elimu ya mlango kwa mlango, vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, machapisho, nyimbo na aina mbalimbali za sanaa," alisema.

Alitaja mkakati wao wa sita ni kuweka mazingira ya kuaminiana kati ya TRA na walipakodi na wa saba ni kukabiliana kikamilifu na magendo nchini kwa kuwa ni mwanya mkubwa wa uvujaji wa mapato ya serikali.

Kayombo aliwashukuru walipakodi nchini kwa kuwezesha kukusanya Sh. trilioni 22.99 na kufikia lengo la asilimia 99.22 ambao ni ukuaji wa asilimia 22.77.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2022/23 wameanza kwa kasi kuelimisha watumishi na wafanyakazi kuhusu mabadiliko ya sheria mbalimbali za kodi, tozo na ada wanazozisimia pamoja na taratibu za kukusanya na usimamiaji wa mapato.

Alisema mabadiliko hayo yamegusa sehemu mbalimbali na sheria za kodi ambazo baadhi ni Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sheria ya Magari ya Kigeni, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sheria ya Madini na Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje.

Alisema kwa mwaka huu wa fedha TRA imepewa jukumu la kukusanya Sh. trilioni 23.65 ambayo ni sehemu ya bajeti ya serikali ya Sh. trilioni 41.48.

Kayombo aliishukuru serikali kwa kuwaongeza watumishi 2,100 ili kuongeza nguvu kazi pamoja na rasilimali mbalimbali.

"Tunaomba ushirikiano wa wadau wote katika mwaka huu wa fedha wakiwamo ninyi waandishi wa habari ili kutuwezesha kufikia lengo lililopangwa kwa ajili ya kuiwezesha serikali kupanga maendeleo ya nchi.

"Ninaomba kutoa wito kwa wananchi wote kujitokeza kuhesabiwa Agosti 23 mwaka huu, ili kuiwezesha serikali kupanga vizuri mipango ya nchi ili tuweze kupata huduma bora zaidi," alihitimisha.




Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, Justus Magongo (kulia), akipokea vitanda 80 vya ngazi mbili na magodoro yake 160 yenye jumla ya thamani ya shilingi milioni 27 kutoka kwa Meneja wa Kanda ya Ziwa wa Benki ya NMB, Baraka Ladislaus, kwa ajili ya Shule ya Msingi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya Kaigara iliyopo Muleba mkoani Kagera jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni tuhuma za kuua mke na mtoto

**Idda Mushi,** MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani Morogoro linamshikilia Msafiri Salum Mdede (33), mkazi wa Tarafa ya Mkuyuni wilayani Morogoro kwa tuhuma za kumuua mkewe na mtoto mdogo wa umri wa miaka mitatu baada ya kuibuka ugomvi wa kifamilia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Musilim, alithibitisha kutokea kwa mauaji hayo Agosti 11 mwaka huu majira ya saa moja asubuhi katika Kitongoji cha Maskati, Kijiji cha Hewe, Kata ya Tegetero, Tarafa ya Mkuyuni, Wilayani Morogoro.

Aliwataja waliouawa kuwa ni mke wa mtuhumiwa, Mariam Vitalis na mtoto wao, Leilah Msafiri , wote wakazi wa kitongoji hicho.

Kamanda Musilim alisema watu hao waliuawa kwa kuchinjwa kwa kitu chenye ncha kali na walipoteza maisha eneo la tukio.

Baadhi ya ndugu wa marehemu Mariam, Ephania Stephen na Justine Izdory, ambao ni kaka wa marehemu, wakizungumza nyumbani kwao eneo la Chamwino, Manispaa ya Morogoro, wamelaani vikali tukio hilo na kuomba sheria ichukue mkondo wake hata kama haitawezekana kurudisha uhai wa wapendwa wao.

Katika hatua nyingine, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro alisema wamewahoji watu kadhaa akiwamo mume na mke ambao ni wakazi wa Ifakara wilayani Kilombero kwa tuhuma za kumwozesha binti yao mwanafunzi mwenye umri wa miaka 17 bila ridhaa yake.

Awali binti huyo mdogo aliwaambia mashujaa wa kukabiliana na ukatili wa kijinsia, SMAUJATA, wilayani Kilombero kuwa hakutaka kuolewa na baba huyo mtu mzima, lakini wazazi wake walipanga kumsafirisha kwenda mkoani Mbeya ambako angeolewa kwa mkopo hadi pale mume mtarajiwa huyo atakapovuna mpunga na kuuza ndipo angelipa mahari.

"Sitaki kuolewa kwa sasa, na mbaya zaidi mwanamume mwenyewe ni mzee, hata ikiwa amri yangu siwezi kuolewa na mzee, lakini kwa sasa sitaki kabisa kuolewa, ndiyo maana nilikwenda kwa hiyari kutafuta msaada kwa mwenyekiti wa mtaa," alilalamika binti huyo katika mahojiano na viongozi wa SMAUJATA Ifakara.

# IGP Wambura amulika kasi upelelezi wa kesi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Jeshi la Polisi, IGP Camillus Wambura, amesema kwa sasa kesi nyingi zilizokuwa zimekwama kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo upelelezi, zimefanyiwa kazi na zilizobaki ni chache.

Wambura aliyasema hayo jijini hapa juzi alipofungua mkutano wa siku mbili wa Wakuu wa Mashtaka wa Mikoa, Wakuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mikoa na Wakuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mikoa.

Aliwahakikishia Watanzania kesi hizo tayari zimeshashughulikiwa na mamlaka zinazohusika na kwamba hadi sasa zipo kesi chache zinapelelezwa.

Alisema ushirikiano uliopo kwenye suala la utendaji, umesaidia kushughulikia upelelezi wa kesi na uendeshaji wa mashtaka.

"Hizi taasisi tatu zina ushirikiano wa karibu sana wa kiutendaji lakini pia zina mawasiliano ya karibu wakati wa upelelezi, uendeshaji mashtaka na kwa ujumla utekelezaji wa haki jinai kwa wananchi wetu.

"Taasisi hizi tatu ushirikiano wetu umeweza kukwamua kesi nyingi zilizokuwa zimekwama kwa sababu ya upelelezi au kesi za kubambikwa.

"Taasisi hizi zipo vizuri na ushirikiano wake ni wa hali ya juu, Watanzania wategemee mambo makubwa sana," IGP Wambura aliahidi.

# Majaliwa asisitiza ushirikiano serikali na madhehebu ya dini

**Na Mwandishi Maalum**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa amesema serikali itaendelea kushirikiana na madhehebu yote ya dini katika nyanja mbalimbali ili kukuza na kuimarisha ustawi wa wananchi kiuchumi na kijamii.

"Sote tumeshuhudia jinsi serikali inavyoweka mazingira mazuri ya kuwekeza kwa ujenzi wa miundombinu muhimu ya barabara na madaraja, reli ya kisasa, vivuko, meli na usafiri wa anga.

"Jitihada hizi zote pamoja na kuimarisha uzalishaji wa umeme, gesi na maji nchini zinafanyika kwa lengo la kuboresha ustawi wa maisha ya Tanzania," Majaliwa alisema juzi wakati wa ufunguzi wa Jengo la Makao Makuu ya Kanisa la Tanzania Assemblies Of God (TAG) katika Chuo cha Biblia Miyuji, Dodoma.

Jengo hilo litakuwa na ofisi mbalimbali za kiutendaji za TAG pamoja na kutoa mafunzo ya uzamili na uzamivu kwa viongozi na wachungaji mbalimbali kutoka Bara la Afrika na maeneo mengine duniani.

"Serikali inaelewa kwamba maendeleo ya nchi yanahitaji ushiriki wetu sote. Tukiimarisha ushirikiano na kila mtu, tutaleta maendeleo ya taifa. Kwa kuzingatia hayo, serikali imekuwa ikishirikiana na sekta binafsi zikiwamo taasisi za dini katika kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi na kuleta maendeleo ya taifa," alisema.

Waziri Mkuu alisema kanisa la TAG pamoja na taasisi nyingine za kidini, zimekuwa mstari wa mbele katika utoaji wa huduma mbalimbali zinazogusa jamii kama elimu, afya na huduma nyingine muhimu kwa jamii ambazo serikali pekee isingeweza kuzifikisha kwa wananchi mara moja.

"Kipekee nilipongeze sana kanisa la TAG kwa kutoa huduma ya elimu kupitia shule zenu za msingi na sekondari ambazo ziko ndani ya mikoa mbalimbali nchini.

"Nimeelezwa mnazo shule za msingi 10 na shule tano za sekondari zilizokamilika na kwamba nyingine nane ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi.

"Hali kadhalika, mnavyo vyuo vya ufundi stadi viwili lakini hamkuishia hapo, sasa manataka kujenga chuo kikuu hapa Dodoma, hongereni sana," Majaliwa alisifu.

Akizungumzia malalamiko ya TAG ya kucheleweshwa kumilikishwa ardhi katika eneo la Chigongwe, Majaliwa alimtaka Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, ahakikishe suala hilo linashughulikiwa haraka na ndani ya siku saba awasilishe taarifa kwake. TAG inataka kujenga chuo kikuu katika eneo hilo.

Askofu Mkuu wa TAG, Dk. Barnabas Mtokambali, alisema kanisa hilo mbali na jukumu la kiroho kuwafanya watu wote waache maasi, pia lina wajibu wa kujihusisha na maendeleo ya kijamii yanayogusa mtu kiroho, kimwili, kiakili, kihisia na kijami.

"Kwa kuzingatia hayo, kanisa la TAG katika mpango mkakati wake wa miaka 13 (2020-2033), limeweka mkakati wa kujenga shule za msingi na sekondari kila mkoa, vituo vya watoto yatima, vituo vya afya kila mkoa, visima wya maji vijijini, vyuo vya elimu na afya, chuo kikuu hapa Dodoma na miradi mingine ya maendeleo ya kanisa na jamii kwa ujumla," alisema.

Askofu Dk. Mtokambali alitumia fursa hiyo kumpongeza Rais Samia kwa kudumisha amani na mshikamano wa kitaifa pamoja na kusimamia jitihada mbalimbali za kuhakikisha miradi yote ya kimkakati inasonga mbele na kuibua miradi mingine mipya.

## Wizara Maji yachota ujuzi Afrika Kusini na Zimbabwe

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Maji imetumia wiki moja Afrika Kusini na Zimbabwe kujifunza masuala ya usafi wa mazingira vijijini, matumizi ya dira za malipo ya kabla kwa wateja wa huduma za maji ili kuimarisha sekta ya maji nchini.

Timu hiyo ambayo iliongozwa na Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, ilikuwa na wataalamu wa sekta ya maji kutoka wizarani na taasisi zake.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dodoma, Naibu Waziri wa Maji, Mahundi alisema lengo la kwenda katika nchi hizo ni kutaka kuimarisha sekta ya maji, pia kuhakikisha watu wa vijijini na mijini wanafikiwa na huduma hizo ili kuondoa malalamiko.

"Tumejifunza vitu vingi sana katika nchi hizo, ninaimani tunakwenda kuiboresha sekta ya maji mijini na vijijini,"Naibu Waziri huyo alisema na kuongeza kuwa ziara hiyo imekuwa njema kwao kwa kuwa nchi hizo zimepiga hatua katika matumizi ya vifaa hivyo.

"Tulibahatika kutembelea kiwanda kinachotengeneza vifaa hivyo na baadhi ya vijiji tulipitia kuviona vinavyotumia mita za malipo ya kabla," alisema.

Alisema miradi wamepangwa kutekelezwa miradi 1,029 kufikia mwaka 2025 ambao ni ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999 na kati yake, miradi 648 inaendelea kutekelezwa huku miradi 381 ni mipya ambayo itaendelea kutekelezwa.

Naibu Waziri huyo alisema utekelezaji wa miradi hiyo utapunguza shida ya kupata huduma ya maji kwa wananchi wa vijijini na mijini.

Alisema wizara hiyo imeidhinishiwa Sh. bilioni 709.9 kwa ajili ya matumizi kwa mwaka huu wa fedha, akisisitiza wanakwenda kuboresha miundombinu ya utoaji huduma za maji vijijini.



Dereva wa bodaboda akiwa amepakia mzigo wa godoro na abiria juu katika Mtaa wa Jamhuri, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, kitendo kinachoweza kuhatarisha usalama wao. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## DED aagizwa kufaya tathmini ya mifugo

**Na Restuta Damian,** MISENYI

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi mkoani Kagera, Projestus Tegameisho, amemwagiza mkurugenzi wake, Waziri Kombo, kufanya tathmini ya mifugo ili kujua idadi iliyoongezeka kwa sasa.

Tegameisho alisema, awali kazi ya kuhesabu mifugo mbalimbali wilayani humo ilikuwa inafanywa na shirika lisilo la kiserikali la World Vision lakini sasa inafanywa na serikali kupitia halmashauri.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akitoa shukrani kwa shirika hilo ambalo limekuwa likitoa huduma za jamii katika wilaya hiyo kwa miaka 26.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, kumekuwa na tabia ya watendaji ya kutofanya mwendelezo wa mazuri yaliyoachwa na mashirika yasiyokuwa ya serikali.

"Tumekuwa na tabia ya kupokea vitu kwa furaha halafu tunaviacha vinaondoka au kupotea kabisa na sisi kurudi nyuma kimaendeleo na kuwa tena wategemezi, lakini mikoa mingine wanafanikiwa," alisema Tegameisho.

Alitaka kuundwa kamati za ufuatiliaji kwa kijiji kimoja hadi kingine ili kuona kazi zilizofanywa na shirika hilo kwa miaka 26.

Alisema kuna vijiji 18 katika kata tano ambavyo vimepatiwa mifugo na mbinu bora za kilimo ili kujiendesha vyenyewe na hiyo ni alama iliyoachwa na mashirika hayo.

"Sitegemei kuona bado kuna wategemezi kwenye jamii iliyopo ndani ya vijiji 18 kwani miaka 26 ya shirika kutoa huduma, najua imesimamia kilimo, mifugo, afya elimu na ujasiriamali," alisema.

Mwenyekiti wa mradi wa shirika hilo wilayani Missenyi, Isaya Kamazima alisema kwa miaka 26 wamehudumia sekta ya kilimo, elimu, afya na mifugo kwa ushirikiano na viongozi wa serikali ndani ya eneo husika.

Kamazima alisema, mradi huo ulifikia wakazi zaidi ya 60,000 kwa kata za Kyaka, Mshasha, Kasambya, Mabale na Kilimilile zenye vijiji 18.

Mkuu wa Wilaya ya Missenyi, Wilson Sakulo alisema miradi iliyoachwa na shirika itaendelea kusimamiwa ili kuenzi na kuendelea kutoa hamasa kwa mashirika.

Alisema serikali inatambua umuhimu wa misaada inayotolewa na mashirika yasiyokuwa ya serikali katika kutatua matatizo ya jamii.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Agizo la Rais kuhusu utunzaji mazingira lisifanyiwe mzaha

**RAIS** Samia Suluhu Hassan wiki hii alifanya ziara ya kikazi katika mikoa ya Nyanda za juu Kusini ya Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa kabla ya jana kuingia Dodoma yaliko makao makuu ya serikali. Katika ziara hiyo pia, Rais Samia alikuwa mgeni rasmi katika kilele cha Maonyesho ya Wakulima, maarufu kama Nanenane yaliyofanyika kitaifa jijini Mbeya.

Pamoja na mambo mengine, katika ziara hiyo Rais alihimiza umuhimu wa Watanzania kutunza mazingira. Hayo aliyasisitiza katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Uwanja wa Samora, Iringa na pia aliposimama katika kata ya Mpunguzi mkoani Dodoma akiwa njiani kutokea Iringa.

Samia aliwaagiza viongozi wa mkoa wa Iringa, viongozi wa dini na kimila kuandaa mpango mkakati wa kutunza vyanzo vya maji na mazingira kutokana na ongezeko la shughuli za kibinadamu ikiwamo kilimo.

Sambamba na hilo, aliwataka wananchi wa mkoa huo kuacha kuchoma miti ovyo kwa sababu kwa kufanya hivyo wanaharibu mazingira pia kuacha kuendesha shughuli za kilimo kwenye vyanzo vya maji, hasa kwenye mito. Aidha, akiwa Mpunguzi, aliwataka wananchi kuacha kukata miti ovyo kwa ajili ya mkaa, jambo ambalo linahatarisha ustawi wa mazingira na viumbe hai.

Kauli hiyo ya Rais mkoani Iringa ilitokana na hali halisi iliyopo sasa kutokana na uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji hasa Mto Ruaha unaotumika kwa shughuli za kilimo. Pia katika maeneo mengi kumekuwa na kasi ya ukataji na uchomaji moto miti kwa ajili ya nishati ya kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia.

Ili kuhakikisha jambo hilo linamalizika na kuleta ustawi wa mazingira, Rais alisema ni jukumu la viongozi kusimama kidete katika kulinda mazingira ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kudhibiti uharibifu wa vyanzo vya maji na ukataji miti na uchomaji moto.

Agizo hilo la Samia limekuja wakati mwafaka kwa sababu uharibifu wa mazingira unaongezeka siku hadi siku katika maeneo mengi nchini. Kwa agizo hilo, Rais ameona wazi kwamba kama hatua thabiti hazitachukuliwa, kuna hatari ya kuwapo janga kubwa katika hifadhi ya mazingira.

Kwa mantiki hiyo, kwa kuwa suala la mazingira ni mtambuka, kila kiongozi kwa nafasi yake aweke kuwa ajenda katika majukumu yake ya kila siku. Hata viongozi wa dini na kimila wanapaswa kuhakikisha suala hilo linasimamiwa kidete.

Rais kama alivyosema mkoani Iringa, kasi ya uharibifu wa mazingira na uchomaji moto ni hatari kwa sababu inaweza kusababisha janga lisilotarajiwa. Tunasema hivyo kwa sababu uharibifu unaofanyika katika Mto Ruaha kwa sababu ya shughuli za kilimo, ni tishio kwa uchumi wa Tanzania siku zijazo.

Mto Ruaha ni chanzo kikuu cha upatikanaji wa umeme katika Bwawa la Kidatu na Bwawa la Nyerere katika bonde la Rufiji ambako kinajengwa chanzo kikubwa cha umeme ambacho kitakazalisha zaidi ya megawati 2000. Kwa mantiki hiyo, kama uharibifu huo utaendelea kufanyika bila kuchukua hatua zozote, ndoto za Tanzania kuwa na umeme wa kutosha kwa maendeleo ya viwanda na uchumi wa taifa kwa ujumla hazitafanikiwa.

Hata uwekezaji unaofanyika katika sekta mbalimbali na juhudi za serikali za kuwavutia wafanyabiashara kuwekeza nchini zinaweza kuwa ndoto iwapo kasi ya uharibifu wa mazingira itaendelea na hatimaye kusababisha upatikanaji wa umeme kuwa wa shaka.

Wahenga wanasema tahadhari kabla ya hatari. Kwa maana hiyo, agizo la Rais Samia kuhusu utunzaji wa mazingira lisichukuliwe kama kauli ya kisiasa bali litekelezwe kwa nguvu zote na kila kiongozi mahali alipo. Suala hilo pia liwe kipimo cha utendaji kwa kiongozi yoyote katika ngazi ya serikali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Elimu mwongozo UVIKO-19 sasa itolewe katika daladala

Na Sabato Kasika

**MWONGOZO** wa Wizara ya Afya wa kudhibiti virusi vya corona, uko wazi ambapo pamoja na mambo mengine, unaagiza vyombo vya usafiri zikiwamo daladala kubeba abiria kulingana na idadi ya viti.

Mwongozo huo pia unaelekeza kila abiria kuvaa barakoa, kunawa maji tiririka na kutumia vitakasa mikono, huku uongozi wa vituo vya mabasi ukitakiwa kusimamia uwapo wa vifaa hivyo na kuhakikisha abiria wote wanavitumia.

Kutolewa kwa mwongozo huo, kunalenga kudhibiti ugonjwa huo nchini, huku Watanzania wakihamasishwa kujitokeza kwa wingi katika vituo mbalimbali vya kutolea chanjo kupata huduma hiyo.

Mwongozo huo pia unawataka wamiliki wa vyombo vya usafiri kuweka vitakasa mikono katika vyombo hivyo na kusimamia uvaaji barakoa, kwa ajili ya kudhibiti ugonjwa huo nchini.

Kimsingi, mwongozo huo unaelekeza mengi ya kuzingatiwa ikiwamo kuepuka mikusanyiko mikubwa ya kijamii, kama sherehe, kisiasa na kidini ili kuwezesha wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi na kijamii na kubadili tabia zao huku wakizingatia mbinu za kujikinga na UVIKO-19.

Hata hivyo, wakati tayari mwongozo huo ukiwa umetoa maelekezo kwa lengo la kunusuru jamii dhidi ya ugonjwa huo, bado baadhi ya watu wamekuwa wagumu kuchukua tahadhari, hasa ndani ya daladala.

Kwa mfano katika usafiri kama daladala, ambako mwongozo huo unaelekeza kubeba abiria kulingana na idadi ya viti (level seat), hali sivyo, kwani bado wanaendelea kujazana kama kawaida, tena kupita kiasi.

Mtindo huo wa kujaza abiria kupita kiasi bila kujali kwamba kuna mwongozo ni wazi elimu inahitajika kwa madereva, makondakta na hata abiria wenyewe, ili waweze kuwa makini wakitambua kuwa ugonjwa huo upo.

Pamoja na kuwapo mwongozo huo, kwa sasa ni jambo la kawaida kuona abiria wamejazana ndani ya daladala, huku wachache tu wakiwa wamevaa barakoa, hali ambayo ni mtihani kudhibiti ugonjwa huo. Ninadhani utoaji wa elimu unaweza kusaidia Watanzania kubadilika, kwani baadhi yao bado hawaoni umuhimu wa kuzingatia mwongozo huo, badala yake wako tayari kujazana ndani ya daladala ili kuwahi kwenye shughuli zao.

Si siri kwamba uhaba wa daladala mkoani Dar es Salaam, unaweza kuwa unachangia kuwapo kwa mrundikano wa abiria katika daladala, lakini pamoja na hayo, jambo la msingi ni kulinda afya, mambo mengine baadaye.

Ingekuwa vyema kwa jamii kuachana na imani potofu, kwani wapo ambao hawaamini kuwa ugonjwa huo upo, wengine wanadai kuwa ni siasa tu au biashara ya Wazungu, hawaoni umuhimu wa kuzingatia mwongozo huo.

Iwapo imani hiyo ikiendelea kuchukua nafasi, inaweza kuhatarisha wengi, hivyo elimu ingetolewa kwa wingi ili kuwabadili wenye mtazamo huo unaoweza kuhatarisha maisha yao na ya wengine.

Ni kweli daladala hazitoshi, abiria wanataka kuwahi kwenye shughuli zao au nyumbani, kondakta naye anataka pesa, matokeo yake ni kutozingatia kile ambacho mwongozo mpya unaelekeza kwa lengo la kudhibiti corona.

Kwa hali kama hiyo, ninadhani kuna jambo la kufanya bila kuathiri upande wowote, ambalo ni kuongeza magari ya abiria kama ilivyokuwa mwaka juzi, ili kupunguza mrundikano kwenye daladala moja. Pamoja na hayo, ni vyema kila mtu kulinda afya yake badala ya kusubiri asukumwe, huku akijua kuwa kinyume cha hapo anaweza kujikuta katika hatari ya kuambukizwa ugonjwa huo na kupoteza maisha.

Kuendelea kuwapo kwa ugonjwa nchini, ndiko ambako kumesababisha wadau mbalimbali kujitokeza na kuanzisha kampeni kuhamasisha na kutoa elimu ya chanjo, inayoitwa 'Tanzania iko Tayari'.

Kampeni hiyo ilizinduliwa jijini Dar es Salaam na inashirikisha wadau kama Africa Union, Access Challenge, African CDC, Jakaya Kikwete Foundation na Clouds Media Group (CMG).

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Tujitokeze kwa wingi kuhesabiwa ili tujipange kimpango mkakati



Na Pascal Mayalla

AGOSTI 23 ni siku ya Sensa ya Watu na Makazi, ni jambo zuri kwa mustakabali wa taifa, hivyo Watanzania tujitokeze kwa wingi kuhesabiwa ili kuiwezesha serikali yetu kutujua tuko wangapi na hatimaye kujipanga kwa mpango mkakati wa kutuletea maendeleo.

Pamoja na hayo, nashauri tusiishie tu kuhesabiana bali serikali yetu itumie sensa kupata mrejesho toka kwa Watanzania, wanataka serikali yao iwafanyie nini. Kwa maana hiyo, matokeo ya sensa pia yaonyeshe matarajio ya Watanzania na mategemeo yao kwa serikali yao.

Serikali pia itoe majibu mujarabu ambayo yatawafanya Watanzania kutimiza wajibu wao wa kufanya kazi kwa bidii na kulipa kodi stahiki hatimaye kuiwezesha serikali kukidhi matarajio yao.

Japo sensa ni mchakato wa kukusanya takwimu juu ya watu kidemografia ili kujua Tanzania tuko wangapi ili kujipanga kimpango mkakati, je, kuna ubaya wowote kama katika hoja za sensa pia tutawauliza Watanzania wangetaka serikali yao iwafanyie nini na wao wako tayari kuifanyia nini Tanzania?

Swali hili liwe la ziada na si la lazima ili kupima kiwango cha matumaini na matarajio ya Watanzania kwa serikali yao na serikali kupata mrejesho wananchi wake wanataka nini, wanategemea nini na wako tayari kufanya nini ili serikali ikidhi matarajio yao na wakati huo huo serikali kujitathmini kama itaweza kutimiza na kukidhi matarajio na mategemeo ya Watanzania.

Hii ni kwa sababu hakuna utaratibu wowote rasmi wa ushirikishwaji wa wananchi kujua wanataka nini kwa nchi yao na mategemeo yao kwa serikali yao, hivyo serikali kuweka wajibu kwa wananchi ikiwamo kulipa kodi kwa hiyari bila shuruti.

Wananchi wakiwa na matarajio fulani kwa serikali yao, serikali nayo ikiwataka watimize wajibu wao wa kufanya kazi kwa bidii na kulipa kodi kwa bidii, watawajibika ipasavyo.

Nimeishi kidogo nchi za wenzetu kama Uingereza, Ufaransa, Uswisi, Italia na Sweden katika majiji ya London, Paris, New York, Geneva, Rome na Stockholm. Maisha kule ni juu, ghali na kodi ni kubwa lakini ni miongoni mwa nchi zenye hali bora za maisha. Wananchi wa mataifa hayo wanatoa matarajio yao kwa serikali zao na serikali zinaahidi kukidhi matarajio yao.

Ili kuyafanya hayo, wanapaswa wawajibike kufanya kazi kwa bidii na kulipa kodi ili serikali ziwahudumie kikamilifu na kutimiza matarajio yao.

Huku kwetu mpaka hadi sasa bado tunakimbizana na kushikana mashati kulipa kodi wakati kwa wenzetu, mtu unajisikia fahari kulipa kodi.

Moja ya sifa ya uongozi ni kuonyesha namna anavyolipa kodi lakini huku kwetu kuonyesha heshima kwa viongozi wetu ni kuwapa misamaha ya kodi.

Wenzetu wana bima ya afya kwa wote, mwanamke akipata ujauzito bila kuolewa, anapewa msaada wa kumlea mtoto.

Mtu akitimiza umri wa kupiga kura au akimaliza shule akakosa ajira ya kuendeshea maisha yake, analipwa mafao ya kukosa ajira.

Pia hifadhi ya jamii ni kwa wote. Ukitimiza umri wa miaka 80, unalipwa mafao ya uzeeni hadi Mungu atakapokuita.

Kwa uchumi wa Tanzania huko tuendako, haya yote yanawezekana kutokana na kuwa na uchumi imara. Sisi Tanzania tuna kila kitu cha kutuwezesha kufikia kiwango hicho.

Ili tuendelee tunahitaji vitu vinne, watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Tanzania tuna watu wengi wa kutosha, ardhi ya kutosha yenye rutuba na yenye vyanzo vingi vya maji. Ina rasilimali za kutosha yakiwamo madini anuwai.

Pia kuna siasa safi na uongozi bora. Pamoja na yote hayo, tujiulize tunakwama wapi?

Kwa maoni yangu kutokana na uzoefu wangu kwa kuishi nchi za wenzetu, kitu pekee kinachotukwamisha Tanzania ni kwenye kupanga mipango yetu.

Tunakosa malengo yenye uhakika hasa kutokuwa na mipango mikakati katika masuala mbalimbali.

Tunapanga mipango mingi ya kitaifa na kuizindua kwa mbwembwe. Mwisho wa siku hatupeani mrejesho ili kuona tulikwama wapi.

Tulikuwa na MKUKUTA, MKUZA, MKUMBITA, MKURABITA, KILIMO KWANZA, matokeo makubwa sasa na sasa tuna DIRA 2025. Tumetekeleza vipi mipango hiyo na mafanikio yake ni kwa kiwango gani?

Niliwahi kusema kwenye moja ya makala zangu kuwa Tanzania tuna tatizo mahali kwenye kupanga vipaumbele vyetu. Tanzania ni nchi inayotegemea kilimo, hivyo kipaumbele cha kwanza kwenye miradi ya kimkakati, ilipaswa iwe miradi ya kilimo.

Wachumi wanaojua kufanya hesabu kwa fedha zilizotumiwa kwenye miradi kama ununuzi wa ndege na ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) wanaweza kutueleza kama fedha zilizotumika zingezamishwa kwenye sekta ya kilimo, tungefika kiwango gani cha uzalishaji?

Kufanya kosa sii kosa, kosa kurudia kosa. Wenye nchi ni sisi twendeni kuhesabiwa, tujipange vyema tupae kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Mimi mwenzenu Mzalendo Pasco Mayalla na familia yangu, tuko tayari kuhesabiwa, Vipi Wewe msomaji wangu?

Natoa wito, Agosti 23 tujitokeze kwa wingi kuhesabiwa na kutoa ushirikiano wote kwa makarani ili kuhesabiwa.

**Mungu Ibariki Tanzania**

**Wasalaam**
**Paskali**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Watanzania bila shaka tumewaona Wakenya uchaguzini



Na Joseph Kulangwa

JAMII zamani ziliongozwa kifamilia na hata kiukoo, na ilikubalika na ndiyo sababu katika jamii zetu za kiafrika, tuliongozwa na wafalme na hata watemi.

Ili mradi kulikuwa na mfumo wa uongozi ambapo koo au familia ziliachiana kwa urithi, akifa kiongozi basi kizazi kilifuatana kuongoza kana kwamba ndicho kiliandikiwa na Mungu kutoa uongozi.

Hivyo Dunia ikaongozwa na wafalme na masultani kwa miaka nenda rudi, lakini hata familia zilizopewa majukumu ya kiuongozi, zilikuwa ni zile zilizojiweza kiuchumi, lakini pia hekima na busara vilichangia.

Kwa maana hiyo, kulikuwa na sifa na vigezo vya kupata viongozi hata kama ilikuwa kwa kurithishana ndiyo sababu mdogo alirithi uongozi hata kama mkubwa alikuwapo. Namaanisha kaka mtu aliweza kuachwa mdogo mtu akachukua uongozi.

Baada ya mfumo wa kurithishana kupitwa na wakati, ndipo ukaja mfumo wa uchaguzi ambapo waongozwa walipiga kura na kupata viongozi wao, safari hii koo hazikupewa nafasi ila kiongozi alitoka ukoo wowote.

Jambo la msingi lilikuwa ni sifa na vigezo kuzingatiwa. Hivyo jamii ilifanya uchaguzi kwa kupiga kura za siri au za wazi, zikizingatiwa sifa alizokuwanazo mgombea. Ni mfumo unaoendelea kutamalaki hadi leo katika jamii nyingi duniani.

Si kwamba urithi wa uongozi umetoweka duniani, la hasha kuna maeneo bado unapewa nafasi, husuan katika baadhi ya mataifa ya Mashariki ya Kati na hata Mashariki ya Mbali. Lakini imetokana na ridhaa ya jamii husika.

Mchakato wa uchaguzi ni sawa na mchezo wa soka ambapo timu hujiandaa na siku ya siku timu mbili hukutana na kupambana kwenye uga na hatimaye mshindi kupatikana na kupewa tuzo yake stahiki.

Katika soka kama ijulikanavyo, kunapokuwa na timu mbili, husimamiwa na mwamuzi na wenzake wanaomsaidia, huku watazamaji wakikaa pembeni mwa uga kushangilia, kila mmoja akiwa na mapenzi kwa moja ya timu zinazonyukana.

Kwenye mchezo kunakuwa na rafu nyingi za kupanga na zingine za bahati mbaya lakini pia zinakuwapo za makusudi na kama mwamuzi na wenzake watakuwa hawaoni, au wameingiwa na ibilisi, kwa namna moja au nyingine, basi ndivyo mchezo nao huingiwa dosari.

Hivi sasa Watanzania tunashuhudia majirani zetu, ndugu zetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wakenya, wako katika kinyang'anyiro cha kupata viongozi wao watakaodumu miaka mitano.

Washindani katika kinyang'anyiro hicho, wanachuana vikali, kwa upana wake tumeshuhudia timu mbili zikichuana; Timu Raila na Timu Ruto, huku wapiga kura ambao ndio washangiliaji, wakikaa pembeni kuangalia nani ataibuka na kombe.

Sisi watazamaji wa upande huu wa Tanzania, tunafuatilia kwa karibu jinsi mechi hiyo ilivyo ngumu, tukiona faulo lakini pia chenga zinazopigwa na timu zote, huku mwamuzi Chebukati na wenzake, wakijitahidi kuona mechi inamalizika salama.

Ikumbukwe, kuwa nasi mwaka juzi tulikuwa na mechi kama hiyo, tukishuhudia Timu Magu na Timu Lissu, zilivyopambana chini ya mwamuzi Semistocles na wenzake, wakifanya yao na hatimaye kushuhudia mchezo uliokithiri rafu na madhambi. Mikono ikicheza badala ya miguu!

Tuliona jinsi wachezaji wa upande mmoja walivyokuwa wakikanyaga wenzao mpaka utosini lakini mwamuzi akionekana kutomudu mchezo na hatimaye wachezaji wa upande mmoja kujikuta karibu wote wako nje ya mchezo nakubaki timu moja tu uwanjani.

Tukikumbuka mechi yetu namba 102020 na tukaiangalia hii ya Kenya namba 082022 bila shaka tunakubaliana kwamba kuna tofauti kubwa sana ya kiuchezaji. Kwani tangu mazoezi, tulishuhudia wachezaji wa pande zote wakijiandaa bila vurugu bila kuingiliwa.

Bahati mbaya sana kwamba baadhi ya timu zetu hazikuruhusiwa kukusanyika kufanya mazoezi, achilia mbali kupita mitaani kunyoosha miguu kwa kutembea au kukimbia, wakiambiwa hakuna mikusanyiko wala maandamano, isipokuwa kwa moja iliyokuwa inatetea ubingwa!

Tukiangalia wenzetu wa Kenya katika mchakato mzima wa uchaguzi, wamepiga hatua kubwa sana ya kidemokrasia aisee, ambako watu wana uhuru wa kukusanyika achilia mbali kufanya mikutano bila kizuizi.

Katika kampeni hatukuona aghalabu watu wakipigwa mabomu wala misafara kuingiliwa na Polisi kwa sababu hii au ile, kwao mikusanyiko haikuwa haramu kama ilivyokuwa hapa. Mara helikopta kuzuiwa kutua, mara majukwaa kukataliwa mikutano ya hadhara.

Lakini kubwa zaidi tuliloona Kenya katika machakato mzima, hakuna mitandao iliyozimwa, ila televisheni kuruhusiwa kurusha matokeo tena kwa kujumlisha wenyewe kwa uhusa ya Chebukati, akisema jumlisheni tu lakini hatimaye Tume ndiye baba la matokeo.

Bila shaka Watanzania tuliokwenda Kenya kuangalia uchaguzi huo, tumejifunza ya kuja kuwafunza wenzetu jinsi ya kucheza mechi hizi kwa uhuru na haki, ili hatimaye tuondokane na Bunge lenye sura ya chama kimoja kama linavyoonekana kutokana na rafu za mechi namba 102020.

**Alamsiki!**

# FEDHA INAPOGEUKA LAANA KATIKA FAMILIA

Na Dk. Enock Mlyuka




FEDHA rasilimali muhimu sana kwa maendeleo ya nyanja zote katika maisha ya mwanadamu. Kwa hali hiyo, kuwa na fedha si dhambi. Fedha hutumika kwa ajili ya mahitaji mbalimbali kama vile kusomesha watoto, ujenzi wa nyumba, mahitaji mbalimbali ya nyumbani na usafiri.

Katika maisha ya sasa bila kuwa na fedha, hasa kwa wale wanaoishi mijini, ni vigumu kupata mahitaji yao ya kila siku. Yote hiyo inaonyesha ni jinsi gani fedha zilivyo muhimu kwa maisha.

Pamoja na umuhimu huo wa fedha, nafasi ambayo mtu anaipa katika maisha yake ndiyo itakayoamua kama ni baraka au laana. Hata kutafuta kwake kama ni kwa njia halali na kutumika vizuri, inaweza kuwa nyenzo muhimu katika kuleta maendeleo. Kinyume cha hivyo, fedha inayo uwezo wa kuleta maumivu na kugeuka kuwa shina la ubaya.

Fedha ina nguvu katika maisha ya mtu binafsi na katika uhusiano na watu wengine. Katika muktadha wa maisha ya ndoa, fedha imesababisha ndoa kuimarika baada ya kupata fedha na wanandoa kufurahia mafanikio. Lakini kuna baadhi ya ndoa zilizoharibika na kusambaratika baada ya fedha kupatikana. Baadhi ya wanandoa wameingia kwenye taabu na majuto licha ya kwamba wanazo fedha. Fedha imegeuka kirusi katika ndoa na uhusiano wa wanandoa.

Utafiti mbalimbali unaonyesha kuwa migogoro mingi ndani ya ndoa imesababishwa na mambo yanayohusu fedha. Matumizi ya fedha yamesababisha matatizo mengi katika ndoa nyingi huku ubinafsi ukielezwa kuzielemea ndoa nyingi. Tatizo linakuwa kubwa hasa pale fedha ya mume inapoonekana haimhusu mke na pia fedha ya mke kutokumhusu mume.

Mfumo dume katika jamii umeongeza ukubwa wa tatizo hili kwani suala la fedha ameachiwa mume bila mke kuwajibika, kujua au kuchangia lolote. Wanawake wenyewe wengi wao wamewaachia waume zao kuwajibika kwa kila kitu kinachohusu fedha na katika maamuzi yote yanayohusu fedha ndani ya ndoa.

Aidha, uamuzi mwingine umeangamiza familia kwa sababu ni mtu mmoja, yaani, mume au baba katika ndoa ndiye hutoa maamuzi kuhusu mambo yanayohusu fedha. Hata hivyo, ni ukweli ulio dhahiri kwamba katika zama hizi mambo yamebadilika.

Suala la fedha limeleta matatizo katika ndoa nyingi za leo. Imetokea kwamba wanandoa waliishi kwa amani kabla ya fedha kupatikana au kufanikiwa kimaisha lakini baada ya kupata mafanikio, wanandoa wamebadilika na kuanza kuumizana.

Mwenzi anaonekana ni mtu asiyeendana na hadhi ya mwenzake. Fedha imependwa zaidi kuliko mwenzi au familia. Hali ya namna hii imesababisha kwa sehemu kubwa baadhi ya wanandoa kutengana na ndoa kuvunjika. Athari zake ni kubwa si kwa wanandoa wenyewe tu, bali kwa watoto waliozaliwa katika ndoa hizo.

Hali hiyo pia huathiri watoto kiroho, kisaikolojia na kimakuzi. Watoto wanakosa haki ya kuishi na wazazi wao kwa pamoja, wanakosa malezi bora ya baba na mama, wanakosa furaha na kujisikia kutokuwa salama (insecure) kwa sababu ya kukosekana kwa baba au mama. Watoto wanarithishwa ubaya ikiwa ni pamoja na roho ya kuoa, kuacha na kuachika.

**FEDHA NA MIHEMKO**

Baadhi ya wababa wakipata fedha ndio mwanzo wa kufanya vitendo vya ukatili katika familia (domestic violence) na unyanyasaji (harassment) kwa wake zao.Uhusiano mpya huanzishwa nje ya ndoa (michepuko) ambapo fedha hupata matumizi makubwa zaidi huko nje kuliko katika familia yake. Hali hii hufisha uhusiano wao na kudumaza ustawi wa ndoa na familia.

Kadhalika wako baadhi ya wanawake ambao wakifanikiwa na kuwa na kipato kikubwa kuliko waume zao, kiburi na dharau huinuka dhidi ya mume. Mahali pengine, mume huishi kama kibarua au mkimbizi ndani ya nyumba yake. Kauli mbaya za mke kwa mumewe huwa jambo la kawaida.

Mke hutumia fedha anavyotaka na kufanya mambo anavyojisikia binafsi bila kumshirikisha mumewe. Akiulizwa anasema hii ni pesa yangu haikuhusu kwani ninao uhuru wa kuitumia nitakavyo.Heshima kwa mume hupungua kama si kuondoka kabisa. Mbaya zaidi, baadhi ya wanawake husahau kutimiza majukumu yao ya kindoa kwa waume zao. Mazingira kama haya yamesababisha hatima na mustakabali wa ndoa nyingi kuwa katika mashaka makubwa.

**NINI KIFANYIKE?**

Ili kunusuru mambo hayo kuendelea na kuleta maafa zaidi, kuna mambo kadhaa yanapaswa kufanywa. Miongoni mwayo ni;-

**MIPANGO NA NIDHAMU**

Mafanikio ya kiuchumi ya mtu yeyote yanahitaji mipango na nidhamu katika fedha. Watu wengi hushindwa kufikia malengo na kufurahia maisha kwa sababu ya kukosa mipango na nidhamu ya fedha. Mpango wowote huanzia kwenye kipato kidogo, si lazima kuwa na kipato kikubwa.

Tabia nzuri ya kujenga na kuiendeleza tangu mwanzo wa ndoa ni ile ya kujipangia bajeti ya familia. Hii husaidia kuelewa ni fedha kiasi gani zinapatikana na kupanga jinsi gani zitatumika.

Katika kufanya hivyo, ni kanuni kuwa matumizi ya fedha yasizidi kipato. Wanandoa waishi kulingana na kipato chao na uwezo wao. Wajilinde dhidi ya mashinikizo na tamaa ambavyo huweza kusababisha waishi maisha yasiyo yao. Moja ya mambo yanayochangia uwapo wa amani na mafanikio katika ndoa ni kuwa na nidhamu katika matumizi ya fedha.

**WATOTO WAFUNDISHWE**

Watoto wasipewe fedha nyingi za kutumia shuleni kila siku. Ni muhimu watoto wafundishwe kuwa, sio wakati wote wanaweza kupata wanachotaka. Kadri wanavyokua, waelekezwe kuwa na nidhamu ya fedha na shukrani kwa Mungu.

Wale wanaoonekana kuwa ni watoto leo, siku zijazo watakuwa ni watu wazima wanaopaswa kujitegemea katika maisha. Maisha wanayoishi leo ni taswira ya maisha yao ya hapo baadaye. Kila mzazi atavuna alichopanda na kuwekeza kwa mtoto wake.

**KUEPUKA USIRI**

Kumekuwa na tabia ya usiri mkubwa miongoni mwa wanandoa juu ya vipato vyao. Wanandoa wengi hawashirikishani kuhusu vipato vyao. Uwazi na ukweli katika mambo ya fedha vimekosekana katika maisha ya wanandoa wengi, inawezekana kwa kukusudia au kukosa ufahamu.

Hali hii imekuwa ikichangia uwapo wa migogoro katika ndoa nyingi, hasa pale mke au mume anapogundua kuwa alifichwa kuhusu jambo fulani. Hali hii inapojitokeza, huondoa tumaini (trust); hudumaza pendo la ndoa na mapenzi; hupoteza hisia chanya,mvuto na kuondoa uhai wa ndoa. Mahali pengine, usiri juu ya vipato umeleta mahangaiko na maumivu makubwa hasa pale mmoja wa wanandoa anapofariki.

Kwa kuzingatia maana halisi ya ndoa na misingi yake, wanandoa wanapaswa kushirikishana na kuelewana juu ya vipato vyao ili kuepuka matatizo yasiyo ya lazima. Ni muhimu wanandoa watengeneze mazingira ya uwazi na ukweli juu ya fedha na mali zao. Wafikirie athari zinazoweza kutokea kutokana na maamuzi ya kuwa wasiri na waongo miongoni mwao.

**UMOJA NA MSHIKAMANO**

Kuishi kwa umoja na mshikamano ni moja ya misingi ya ndoa bora. Hata hivyo, wako wanandoa wanaofanya vitu au mambo yao pasipo umoja wala mshikamano. Mfano, imetokea mahali pengine kwamba, mke au mume anaweza kununua kiwanja, kununua gari, kujenga au kununua nyumba, kukopa fedha benki, kusaidia ndugu kifedha au kuanzisha mradi fulani bila mwenzi wake kujua.

Inapogundulika, hali hii husababisha masononeko na mgogoro mkubwa. Yafaa mume na mke waishi kwa umoja na mshikamano kwani hii huleta maana halisi ya wao kuwa wanandoa.

**KUPENDA MAZUNGUMZO**

Wanandoa wazungumze kuhusu tofauti zao na kushirikishana hisia walizonazo kwa lengo la kusaidiana na kurekebisha hali iliyopo. Kuishi na machungu moyoni huathiri afya ya akili, mwili hata kusababisha kifo. Kuweka vinyongo moyoni hushawishi visasi. Siku zote vinyongo na roho ya visasi sio njia nzuri ya kutatua tatizo.

Hali hii huwa haileti suluhu, bali huongeza maumivu, huondoa utu na uwepo wa Mungu katika maisha ya mtu. Moja ya mambo yanayochangia watu kuumizana na mauaji ya kikatili katika familia na jamii yetu ni uwapo wa watu wenye vinyongo ambao hukusudia kulipiza kisasi kwa wenzao.

Ili kuepukana na matatizo kama haya ni muhimu wanandoa wadhamirie kujenga tabia ya kupenda kujadiliana kwa upendo na upole na kushauriana kwani mazungumzo hujenga uhusiano na familia bora. Pale wanandoa wanaposhindwa kushughulikia tofauti zao, ni busara kuomba msaada wa viongozi wa dini au washauri wengine wenye weledi ili kutunza ustawi wa ndoa, familia, afya njema ya akili, mwili na roho.

Fedha ni njema na mtu kuwa nayo siyo uovu wala dhambi. Nafasi unayoipa fedha katika maisha yako ndiyo itakayoamua kama fedha ni baraka au laana. Fedha ni baraka ikitafutwa kwa halali na kutumika vizuri, kwani fedha inaweza kuwa nyenzo ya kuleta maendeleo pale itakapotumika vizuri kwa mambo yenye manufaa. Hata hivyo, fedha inayo uwezo wa kuleta maumivu na kugeuka kuwa shina la ubaya isipotumika vizuri.

Wanandoa wajihadhari ili fedha wanazopata zisiondoe utu, heshima na thamani miongoni mwao. Ikumbukwe kuwa, thamani ya mtu haipimwi kwa uwingi au uchache wa fedha alizonazo, bali kwa yale anayowatendea binadamu wengine. Ni maombi yangu kwa Mungu kuwa, fedha ulizonazo zikufanye kuwa baraka katika familia yako na jamii.

**■Dk. Mlyuka ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

AGOSTI 14, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana

# MAISHA
## Jumapili



Ukurasa 13

**Kuwa mtanashati**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Namna bora ya kupangilia mwonekano wa nyumba



Ukurasa 12

**HARUSI**





# Tabasamu pana

Ukurasa 14

## WATOTO

### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA








| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | S | H | A | K | A |
| ■ | U | ■ | ■ | I | ■ |
| A | K | A | ■ | B | ■ |
| ■ | A | ■ | P | A | O |
| ■ | R | ■ | ■ | L | ■ |
| P | I | M | B | I | ■ |

### AMSHA AKILI

TAU KALETEWA ZAWADI, MSAIDIE AIPATE



### TOA TOFAUTI 5




### FUMBO TOTO

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | | | | | |
| ■ | | ■ | ■ | | ■ |
| | | | ■ | | ■ |
| ■ | | ■ | | | |
| ■ | | ■ | ■ | | ■ |
| | | | | | ■ |


Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi: DAU, AMA, TAMBI, JAZWA, WAKATI, JAMBIA

## PAKA RANGI



@A.MSAMBA

## CHEKA



Alichokifanya daktari

JOHN alimtumia ujumbe mdogo wake kuhusu sifa ya jiji la Dar es Salaam kuishi ambako amehamia hivi karibuni.

Ujumbe huo ulisomeka kama ifuatavyo “kuku anachinjwa Kinondoni, shingo inaliwa Tandale, Kidari Masaki, paja linaliwa Mikocheni, firigisi Magomeni, miguu inapendwa kutafunwa Mbagala, kipapatio huwaambii kitu Tandika, kichwa Manzese na utumbo Buguruni. Acha chezea maisha ya Dar wewe.

### CHEMSHA BONGO

Kuna majiko mawili,sufuria mbili zenye kiasi sawa cha maji na majiko yote yamewashwa kwa viwango sawa. Sufuria ya kwanza ina yai moja, sufuria ya pili ina mayai 15.

Je ni yai moja au mayai 15 ndio yatawahi kuiva?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Waganga wa jadi walivyoua mwelekeo wa maisha yangu

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kudadavua vituko vya Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki iliyopita nilikuletea kisa cha shangazi aliyejifungua boga badala ya mtoto. Ni kisa cha kweli kwani kijana aliyenisimulia huyo alikuwa ni shangazi yake.***

Sasa kijana huyo aliyejitambulisha kama Celestine, anaeleza mkasa wake mwenyewe uliomkuta mwaka 2011 na kuharibu hatma ya maisha yake hadi leo. Ana umri wa miaka 42, ana mtoto mmoja aliyezaa na mwanamke ambaye waliachana na kuondoka na mtoto huyo kwenda kwao Iringa. Naye akabaki Mikumi mkoani Morogoro akibangaiza, anakosa hata hela la kula. Hebu tumsikilize.

Anasema: Kisa hiki kinanihusu mimi na rafiki yangu aitwaye Fredy. Mwaka 2011 kutokana na changamato za maisha, tukaona wale wenzetu tuliosoma nao wana maisha mazuri, wana magari, wamejenga nyumba lakini sisi tumedata. Tukamtafuta dada mmoja aitwaye Maria na kumwuliza siri ya maisha yake mazuri.

Maria akatuambia msitegemee tu kazi, bali na njia ya pili ambayo ndiyo rahisi ya kwenda kwa waganga. Mimi nikamwambia Fredy tusiwatafute waganga wa hapa Tanzania bali twende Burundi kule wako waganga wa uhakika. Tukapanga safari kwenda Burundi kwa kuwa alikuwepo mganga tunafahamiana aliwahi kuja kwetu shangazi yangu alipozaa boga akatufanyia uganga.

Baada ya hapo tuliondoka tukaenda Burundi. Tulipofika tukaonana na mtoto wa mganga, tukamuuliza mtaalamu tumemkuta? Akatujibu hapa alishahama. Akatuuliza tumetokea wapi tukajibu Tanzania.

Akasema kama mnayo nauli mnilipie niwapeleke Rwanda kwani kwa sasa anafanyia kazi zake huko. Tukashauriana na kuafiki kwamba tumlipie nauli. Siku iliyofuata tukapanda basi tukafika saa nane mchana.

Muda wa saa tisa tukabahatika kuonana na mganga yule. Kwa kuwa mimi ndiye niliyekuwa nafahamiana naye, nikaanza kumkumbusha kama yeye anankumbuka. Akasema tunavyoongea hivi sasa siwezi kukumbuka ila nikikaa kwenye mtambo wangu nitakukumbuka.

Ila akasema siyo vibaya ukinikumbusha. Nikamwambia uliwahi kuja Tanzania mkoani Kigoma na yupo mama mmoja alijifungua boga. Akasema: Aaaah! Nishakumbuka, sasa tuingie ofisini ili nipate kujua shida zenu ni nini?.

Pale ofisini tulipoingia screen kubwa mfano wa televisheni ukutani. Ukiingia inakudaka na unajiona picha yako ipo ndani yake. Yaani unajiona kama unaangalia TV vile. Baada ya hapo akasema sasa nimeshajua shida zetu.

Mganga alipoanza kutuita mmoja mmoja, alianza na Fredy. Akaambiwa kwamba hawezi kumfanyia huduma hadi amwangalie nyota yake. Akamuuliza upo tayari nikuangalie nyota? Akajibu, niko tayari. Akamwambia avue shati abaki na suruali. Akamwambia nyota yako ni nzuri, sasa upo tayari nikupe masharti sasa hivi? Akamjibu ndiyo nipo tayari.

Mganga akamwambia toka sasa hivi uende mtaani pita nyumba hadi nyumba na ukimkuta mwanamke anapika ugali nje, hakikisha unachukua mwiko anaopikia, tena usiuoshe, uje nao hivyo hivyo na ugali wake. Sharti la pili, kanunue kuku mtetea mwenye rangi nyeupe au nyekundu.

Sharti la tatu kwa Fredy, ukishampata huyo kuku utaamka saa nane ya usiku utaenda naye njia panda au round about (mzunguko wa barabara), utamchinja huyo kuku, huku ukiwa hujavaa nguo yoyote. Kisha utakaa muda usiopungua dakika 10 au 20 ukiwa unatazama Mashariki.

Atakuja mtu atamchukua yule kuku na usimsalimie. Akishainama kuchukua, utamfuata kwa mwendo wa dakika 20. Sharti la nne, utakaporudi, utaamka asubuhi utamtafuta chura hasa wale wanaokaa ndani au chini ya ndoo ya maji au mtungi. Ukishampata utafunga mkono wako kitambaa cheusi halafu ununue wembe mpya. Utampasua huyo chura katikati halafu chukua sarafu ya Sh.100 au Sh.200, kisha iweke katikati ya tumbo la chura.

Kisha chukua chungu au kikaangio cha mboga, mfunikie humo huyo chura kwa siku tatu na utamfunua siku ya tatu kuamkia siku ya nne saa saba kamili usiku. Utakachokutana nacho usiogope, usikimbie, usipige kelele na wala usimwambie mtu yoyote!

Ukimaliza hilo zoezi uende Tanzania au tafuta hapa Rwanda maji ya maiti, kisha unywe nusu lita asubuhi, mchana na jioni. Na utafanya hivyo muda wa siku tatu na ya nne utakuja hapa nikupe maelekezo ya kufanya.

***Hayo yalikuwa ya Fredy, wiki ijayo tutasikia masharti ya Selestine. Una maoni, Kisa? Ujumbe 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Jitihada zinahitajika kukabili magonjwa yasiyoambukiza

WIKI iliyopita Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ulifanya mkutano na waandishi wa habari kueleza utekelezaji wa majukumu, mafanikio, matatizo na ushauri wa namna ha kukabili.

Mfuko huo wenye takriban wanachama milioni 4.8, unahudumia Watanzania asilimia nane huku asilimia sita wakihudumiwa na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na wengine bima za sekta binafsi.

Tunapozungumzia bima ya afya, wengi huurejelea mfuko wa NHIF na ndiko watu wanatamani kujiunga lakini kwa sababu ya changamoto za kipato, wameshindwa kufikia lengo. Wengi wanalazimika kutumia fedha taslimu wanapougua.

Kwa sasa serikali imeahidi kuja na bima ya afya kwa wote, yaani kila Mtanzania awe na bima. Akifika hospitalini anatibiwa moja kwa moja na si lazima hadi awe na fedha taslimu.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, katika mkutano huo na wanahabari alisema mfuko unaelekea kuelemewa kutokana na kuongezeka kwa watu wanaougua magonjwa yasiyoambukiza kama vile figo, sukari, shinikizo la damu na saratani.

Aidha, alisema bila serikali kuchukua hatua na kuja na afua zitakazosaidia Watanzania, kuna hatari ya mfuko kushindwa kubeba huo mzigo mzito wa gharama za matibabu.

Alitolea mfano kwa mwaka 2021/22, zaidi ya Sh. bilioni 99 sawa na asilimia 18 ya mapato ya NHIF, zilielekezwa kwenye matibabu ya magonjwa yasiyoambukiza.

Katika kusafisha damu, kwa mfano, alisema mgonjwa wa figo kwa siku anatumia kati ya Sh. 240,000 na 250,000 na anatakiwa kufanya mara tatu kwa wiki, ambayo kwa mwaka ni sawa na Sh. milioni 52.

Kwa hali ya kawaida, wananchi wengi hawawezi kumudu gharama hizi. Wengi wanapoteza maisha si kwa sababu muda wao wa kuishi duniani umeisha bali kushindwa kumudu gharama za matibabu.

Kwenye taarifa hiyo, Konga alisema ikiwa Watanzania wengi watajiunga kwenye bima na kufikia asilimia 90, ni rahisi kumudu gharama za matibabu, huku akitolea mfano wa nchi zilizoendelea.

Nchini kwetu wengi ambao wako NHIF ni watumishi wa serikali na wachache sana wa sekta binafsi. Wako wanaotamani kuwa na bima ila kutokana na hali ya umaskini wanashindwa kumudu na wengi hupoteza maisha.

Alichokieleza kuhusu magonjwa yasiyoambukiza ni muhimu sana kikapewa msukumo wa kitaifa. Sekta ya afya na familia zinaelemewa na mzigo wa matibabu, hivyo lazima kuja na mbinu za kuzuia.

Mara kadhaa wataalam wameeleza namna mtu anaweza kuepukana na magonjwa hayo ambayo mengi ni mfumo wa maisha, yaani kutokufanya mazoezi, kula ovyo na kemikali zinazoweza kuepukika.

Kama ilivyokuwa kwenye kuhamasisha watu kufanya usafi, basi kuwe na kampeni maalum ya watu kufanya mazoezi kwa faida yao na taifa lao kwa kuwa nguvu kazi ikipungua hata uzalishaji utapungua na nchi itakosa mapato.

Kwa sasa zinafanyika marathoni ambazo ni za kulipia na huusisha wachache, sasa ni wakati wa kuja na kampeni ya kitaifa ya kila wiki kufanya mazoezi, kuwa na maeneo maalum ya mazoezi ili kuwafanya wengi kushiriki.

Lakini ni muhimu kuangalia suala la chakula hasa dawa za sumu ya wadudu zinazopulizwa kwenye mazao na watu kuyatumia pasipokujua, mathalani mahindi yanahifadhiwa kwa dawa ili yasiliwe na wadudu mfanyabiashara bila kujua anasaga anauza unga kwa watu.

> **Alitolea mfano kwa mwaka 2021/22, zaidi ya Sh. bilioni 99 sawa na asilimia 18 ya mapato ya NHIF, zilielekezwa kwenye matibabu ya magonjwa yasiyoambukiza.**

Pia tumeona mboga zikipulizwa dawa na siku chache kupelekwa sokoni, zingine hupulizwa dawa za kuzistawisha na kisha zinauzwa watu wanakula kwenye hoteli hadi nyumbani.

Kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu wanatumia kemikali ya zebaki kuchenjua ambayo inaingia kwenhe mazingira watu wanakula mboga,samaki na viumbe wengine,ambavyo mwisho wa siku wanapata maradhi.

Tayari imethibitika kuwa zebaki husababisha saratani ndiyo maana mikoa ya kanda ya Ziwa ambako kuna matumizi makubwa ya kemikali hiyo inaongoza kwa watu wanaougua saratani.

Mtu anayeishi Dar es Salaam anaweza kuona madhara hayatampata lakini sote tunakula samaki kutoka Ziwa Victoria, lakini maji yanasafiri kutoka eneo moja hadi jingine na sote tunayatumia.

Ni rahisi sana kwa vimelea vya kemikali kupenya kupitia mazingira na vitoweo hivyo alafu mtu anapokula vinajikusanya na kusababisha madhara ya muda mrefu kwake,hivyo nawaza kwa sauti kuwa ni lazima hatua zichukuliwe kuliokoa taifa dhidi ya maradhi haya.

# HARUSI





Agosti 6 mwaka huu ilikuwa siku ya furaha kwa Franco Herman Mwangingo na Imelda Joanes Kyuki, baada ya kula viapo vya uaminifu katika ndoa yao iliyofungwa katika kanisa la Katoliki Gargan Khughung mjini Dodoma. Sherehe ya aina yake ya kuwapongeza ilifanyika katika ukumbi wa Landmark kesho yake.











# MITINDO



# Kuwa mtanashati

MWANAUME aliyevaa kinadhifu zaidi na kwa muonekano wa kitanashati na kupendeza siku zote lazima atatupiwa jicho la ziada

Vizuri kuendana na mitindo ya kisasa na kuwa na aina pekee ya uvaaji ambao utakupa utu na heshima.

Mwanaume anayetamani kuwa tofauti kila siku ni lazima kuzingatia aina zifuatazo za mitindo kwa nia ya kukuweka nadhifu.

### Nguo inayoendana na mwili

Kitu ambacho unaweza kufanya mabadiliko kwenye nguo zako ni kuzipunguza kuendana na mwili wako, usiipunguze ikakubana sana au ikapwaya sana. Ili ikutoe kiutanashati lazima iendane kwa jinsi mwili wako ulivyo.

### Vaa kawaida

Hakuna kitu kinachopoteza utanashati wako hata kama nguo iwe nzuri kama kuvaa nguo bila mpangilio, ukivaa nguo usivalie vito vingi, kuweka pete nyingi na mikufu mingi shingoni utaonekana limbukeni.

Kama ukitaka kuonekana umependeza vaa nguo katika hali ya kawaida.

### Kuwa mwangalifu

Sweta zingine huwa ni kubwa mno au zinakuwa zimekubana kupitiliza, ili utoke bomba mwili wako juu na chini unapaswa uendane, kama umevaa bwanga juu, basi na chini vile vile nguo unayotakiwa uvae inatakiwa iendane na ya juu.

### Usichukulie pupa vitu vidogo

Angalia shati lilivyokukaa, kama umevaa skafu angalia inavyoendana na nguo. Kama ni tai angalia jinsi ulivyoifunga, unaweza kuwa unatembea kumbe mifuko imetoka nje, na kama hujui kufunga tai ni vizuri ukamtafuta mtu mwenye utaalamu huo akufungie.

### Usivae matangazo, nembo kubwa

Unapokuwa unavaa nguo yenye nembo kubwa au tangazo unakuwa kama ubao wa matangazo ya kulipia, unashusha thamani yako na muonekano wako kwa ujumla, tsheti za makampuni haziwezi kukamilisha unadhifu wako, vaa tisheti yenye v kwenye shingo na piga jinzi yako kwa muonekano murua zaidi.

UREMBO



TABASAMU PANA

# Meno meupe hukupa furaha

BAADHI ya meno meupe yenye afya ni ufunguo wa tabasamu zuri, hata kama hutazungumza yenyewe yanaongea.

Iwe mwanaume au mwanamke kitu cha kwanza cha kutambulisha muonekano wako ni tabasamu linalotoka kinywani mwako.

Kwa miaka mingi ni kawaida kuona jinsi meno hupoteza urembo wa asili wa weupe na kuanza kutia giza kama matokeo ya vitu tofauti.

Lakini kuna njia za kuzuia madoa kwa meno meupe, kitu ambacho watu wote wanapenda kuonyesha tabasamu kila siku.

Zipo njia kadhaa za kuzuia madoa hayo kwenye meno meupe ikiwa madoa yametokea bila wewe kujua.

Lakini kabla ya kutibu tatizo ni muhimu kuepuka sababu kadhaa ambazo husababisha madoa ikiwamo kutosafisha kwa mswaki na dawa.

**Tumia Limao kusafisha**

Ikiwa meno yako yanaonekana ya njano kidogo, inaweza kusababisha kubadilika rangi na kuwa meusi kabisa. Hakikisha unachukua hatua za haraka kuyatibu kabla ya kubadilika rangi kabisa na kuwa meusi.

Hatua ya kwanza chukua limao kamua maji yake weka kwenye chombo kisafi.

Chukua maji ya limao na weka mdomoni na uache kwa muda kidogo.

Baada ya dakika tano chukua mswaki na anza kusafisha taratibu meno yako.

Rudia hivyo mara tatu kwa wiki na utaanza kuona mabadiliko kwenye meno yako.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Utamu wa vipopoo

VIPOPOO ni chakula kinachoandaliwa kwa unga wa ngano na tui la nazi.

Ni chakula kitamu sana kutokana na uwepo wa sukari nyingi.

Ni vizuri kula chakula hiki mara chache, hasa baada kupata mlo tofauti ili mwili uweze kuhimili ongezeko la sukari kwenye damu kwa ghafla.









**Mahitaji**

Unga wa ngano nusu kilo, maji vikombe vitatu, chumvi nusu kijiko cha chai, mafuta ya kula, tui la nazi zito vikombe vitatu, iliki kijiko kimoja cha chai na sukari vijiko vitatu vikubwa.

**Maelekezo**

Weka maji na chumvi kwenye sufuria kisha bandika jikoni. Acha yachemke hadi yatokote. Weka unga kwenye maji yanayochemka kwa dadika tano kisha songa kama ugali kwa kutumia nguvu kiasi maana huu unga ni mgumu tofauti na ugali wa kawaida.

Songa kwa dakika 15, kisha mimina kwenye sinia.

Paka mafuta ya kula mikononi na kanda unga. Kata vidonge vidogo vya wastani vya duara, ukifanya hili zoezi usiweke mafuta au unga mkavu na rudia zoezi mpaka unga uishe.

Ukimaliza kukanda, anika juani mpaka vikauke(ingawa si lazima kuanika). Ukianika asubuhi unaweza kupika jioni.

Weka tui la nazi na iliki kwenye sufuria, bandika jikoni na acha vichemke hadi vitokote. Mimina vipopo kwenye sufuria yenye tui la nazi. Punguza moto, acha viive kwa dakika 30. Weka sukari huku ukikoroga.

Baada ya dakika 5 unaweza kuepua na kujiramba wewe na familia yako.

Pishi la leo limeandaliwa kwa msaada wa blog ya misosi.

## MAISHA NI NYUMBA
Na Elizabeth Zaya

## Namna ya kuchagua chupa ya chai




NDANI ya nyumba haikosekani chombo muhimu kwa ajili ya kuhifadhi vinywaji vya moto kama chai au kahawa.

Chupa ya chai ni chombo kinachojulikana na wengi kwa kazi hiyo na kila nyumba huikosi kuiona ikiwa imehifadhiwa ndani ya kabati au juu ya meza ya chakula.

Kama unataka kununua chupa ya chai unatakiwa kuwa makini ili kupata iliyo bora na yenye uwezo wa kutunza joto kwa muda mrefu.

**ANGALIA UVUJAJI**

Kwa kuchagua chupa ya chai, lazima ufanyike uchunguzi ili kubaini haivujishi hewa ndani ya yai lake. Mchukue mtu anayejua vyema chombo hicho ili akusaidie kufanya uchunguzi.

**KUTUNZA JOTO**

Muda wa kuhifadhi joto ni jambo muhimu kwa chupa iliyo bora. Tumia maji ya moto kufanya majaribio ya kuhifadhi joto na kama ukiona maji yanapoa haraka, basi chupa si bora unatakiwa kuirudisha.

**HARUFU**

Wakati wa kuchagua chupa ya chai ni muhimu kufungua. Ni lazima kutoa harufu yote mbaya na kama inaendelea kuwepo basi si salama kwa afya.

**CHUPA YA CHUMA**

Wakati wa kuchagua chupa lazima kutikiswa. Wakati huo yai linatakiwa liwe salama, vinginevyo unashauriwa kununua chupa ya chuma laini kwani ina uwezo zaidi wa kutunza joto.





# Namna bora ya kupangilia mwonekano wa nyumba

BAADA ya miaka kadhaa ya kuishi kwenye nyumba, wengi hutamani kubadilisha mwonekano.

Mara nyingi wamiliki wengi wa nyumba hupendelea kurekebisha jengo au kununua samani mpya ambazo hutumia gharama kubwa.

Si vibaya kufanya hivyo lakini hata pale bajeti inapokuwa ndogo, unaweza kufanya maboresho hayo.

Miongoni mwa vitu ambavyo unaweza kuvitumia kubadilisha mwonekano wa nyumba yako hata bila kutumia gharama kubwa na ikapendeza ni pamoja na namna ya kuchagua rangi ya ukuta.

Nyingine ni matumizi tofauti ya karatasi za ukutani na malighafi zingine zilizotumika kutengenezea samani zako. Vitu hivi vikitumiwa vizuri, vina nafasi kubwa ya kubadilisha kabisa mwonekano wa nyumba yako na kuvutia zaidi.

Kwa mfano, kupaka rangi upya kabati la luninga, miguu ya kiti au meza, kubadili kitambaa kilichotengenezea viti au sofa,nako kunasaidia kubadilisha mwonekano katika nyumba yako.

Nyingine ni kubadili vitu kidogodogo kama vile tai na fimbo za pazia, pazia zenyewe, zuria, mapambo ya ukutani na mengineyo.

Vipo vitu vingi ambavyo unaweza kuvifanyia marekebisho kwa gharama ndogo ndani ya nyumba yako na ukaifurahia tena na usiichoke.

Pia hata kuchagua kubadili kitu kingine unachoona unatakiwa kufanya hivyo. Kama ni foronya unatakiwa kuangalia zile zinazoendana na zilizoko kwa wakati wa sasa.

Kama vitu vyako vya ndani umevitumia kwa miaka mingi na vimepitwa na wakati na ndiyo maana huenda vinakuchosha na kuiona nyumba yako mbaya, usiikatie tamaa kwa sababu inawezekana kuirudisha katika ubora wake.

Kikubwa ni kuwa mbunifu na kuongeza kidogokidogo vionjo vinavyoendana na wakati katika nyumba yako hiyo, hata kama huna kipato kikubwa inawezekana, si lazima uweke vyote kwa pamoja, lakini kadri unavyojaaliwa unabadili cha zamani na unaweka kinachoendana na wakati wa sasa.


Utanunua pazia leo lakini siku nyingine kitu kingine na hii pia itasaidia nyumba yako kuonekana mpya kila siku.

Ni ukweli kuwa vitu vya nyumbani vinabadilika kila baada ya kipindi kifupi, zuria ulilonunua miaka mitano iliyopita, haliwezi kuendana na wakati huu.





# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA 2022
NA MUHIDINI MSAMBA
0656 122770 SMS
...HADUBINI...
KULIKONI MUME WANGU!?
KIPIGO CHA JANA
KASHESHE
JANA MIMI NA MUME WANGU TULIENDA KUPIMA UKIMWI MAJIBU YAMEONYESHA TUPO SAFI
HEHEHEHE... HALOOO HALOO MIMI MZIMA WA AFYA SIAMINI!
INAMAANA TUMEKUPIMIA!?
HABARI NDIYO HIYO
KITAA CHA KWETU
TIMU LANGU LIMENIANGUSHA SANA NATAMANI KULIA, YANI HELA YANGU YOTE IMEMEZWA NA KUBETI
UKIZUNGUMZIA KUHUSU JANA NAKUPANDISHIA KODI YA NYUMBA
MWENYE NYUMA WANGU VIBAYA HIVYO
NDANI YA KIBASI
WEWE DEREVA VIPI HUO MWENDO GANI
MWENDO HADI TUNAPIGA CHIAZI NA MAWINGU
KAMA HAUNA FAMILIA WENZIO TUNAFAMILIA
HUYU ATAKUWA ANASHIBIKIA TIMU ILIYOPIGWA JANA
ATAKUWA ANAISHI GETO MSOSI KWA MAMANTILIE, NDIYO MAANA ANA ROHO NGUMU KAMA CHUMA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...CHUMVI HAIWEZI KUWA SUKARI...

HABARI KIMATAIFA

# Matokeo ya urais yanukia Kenya

**NAIROBI,** KENYA

MATOKEO kutoka maeneo 49 kati ya 292 ikiwamo kura zilizopigwa ughaibuni na magereza yamepokewa kwa ajili ya kuthibitishwa na kutangazwa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC).

Maofisa wa uchaguzi 291 wa majimbo ya ubunge wamefika katika kituo cha kitaifa cha kuhesabu kura Bomas mjini Nairobi ambako waliwasilisha nakala halisi za fomu 34A kwa msimamizi mkuu wa uchaguzi, Wafula Chebukati.

Hata hivyo, IEBC iliripoti kuwa mmoja wa maofisa wake wa uchaguzi ametoweka.

Imelazimu naibu wa ofisa huyo kutoka Embakasi Mashariki jijini Nairobi aliyepotea, kupokea majukumu.

Kuna maeneo 292 nchini Kenya yanayojumuisha Wakenya wanaoishi magereza.

IEBC itatangaza matokeo ya urais baada tu ya kupokea na kuthibitisha matokeo na nakala halisi za fomu 34 A kutoka vituo vyote 46,229 vilivyowekwa kwenye gazeti rasmi la serikali.

Matokeo rasmi yanapaswa kutangazwa ndani ya siku saba baada ya siku ya kupiga kura.

Viongozi wa Muungano wa Azimio la Umoja wakutana

Viongozi wapya waliothibitishwa ushindi katika uchaguzi mkuu Kenya kutoka Muungano wa Azimio la Umoja wa mgombea urais Raila Odinga wamekutana jana katika mji mkuu Nairobi.

Viongozi hao walionekana kumiminika katika jumba la mikutano KICC Nairobi Jumamosi mchana katika hafla ya kutambuana na kutoa pongezi kwa waliotangazwa ushindi katika uchaguzi mkuu nchini humo.

Ni mara ya kwanza mkutano wa Azimio unafanyika tangu wakenya kupiga kura siku ya Jumanne.

Baadhi ya viongozi katika hafla hiyo walikuwa wakizungumza kwa matumaini ushindi wa mgombea urais Raila Odinga, licha ya kukiri pia kushindwa kwa baadhi ya viongozi wakuu waliokuweko.

Akihutubia mkusanyiko huo, mgombea mwenza wa Odinga, Martha Karua alieleza kwamba ni lazima walinde utaratibu unaoendelea katika ukumbi wa Bomas ambao ndio kituo kikuu cha kuhesabia kura nchini humo ili kuhakikisha hauingiliwi.

Alisema matumaini yake kwamba muungano huo utakuwa na uwingi bungeni kwa namna matokeo yanavyoendelea kutiririka.

Kadhalika Martha amekiri kuwa wapinzani wao wanaelekea kuwa na ushawishi katika bunge la Seneti.

BBC

# Salman Rushdie bado yu mahututi

**NEW YORK,** MAREKANI

HALI ya wasiwasi imetanda Marekani baada ya mwandishi wa fasihi, Salman Rushdie, kuelezwa hali yake bado mahututi baada ya kuchomwa kisu.Taarifa zinaeleza tukio hilo lilitokea mjini New York na hali yake ni mahututi licha ya kufanyiwa upasuaji baada ya kukimbizwa hospitalini.

Shambulizi dhidi ya Salman Rushdie lilitokea juzi alipokuwa jukwaani akianza kutoa mhadhara katika taasisi ya Chautauqua.

Mwandishi huyo wa fasihi mwenye umri wa miaka 75 alipangiwa kuzungumzia uhuru wa wasanii mbele ya hadhara ya mamia ya watu. Hata hivyo ghafla alivamiwa na mtu aliyefunika uso kwa barakoa na kumshambulia kwa kisu.

Maofisa wa polisi waliokuwa katika ukumbi huo waliingilia kati na kumtia mbaroni mshambuliaji.

Gavana wa New York, Kathy Hochul amelilaani shambulizi hilo, na aliarifu kuwa Rushdie bado anaendelea kupigania maisha yake akiwa hospitali.

Hata hivyo, hali ya afya yake, imearifiwa kuwa anapumua kwa kutumia mashine, na amepata majeraha mabaya usoni, shingoni na tumboni.

Polisi walisema bado hawajajua malengo ya mshambuliaji wake, wala kubainisha aina ya silaha aliyoitumia.

Hata msemaji wa Salman Rushdie, Andrew Wylie alisema kupitia taarifa ya baruapepe kuwa mwandishi huyo anafanyiwa upasuaji bila kutoa maelezo zaidi.

Rushdie alizaliwa mjini Mumbai nchini ndia katika familia ya Kiislamu kutoka Kashmir, lakini alihamia Uingereza.

Maisha yake yalibadilika baada ya kuandika kitabu cha riwaya alichokiita, Satanic Verses, maana yake, Aya za Kishetani, ambacho Waislamu wengi walikishutumu kuwa na maandishi yanayomkashifu Mtume Muhammad na kuukufuru Uislamu.

Baada ya kuchapisha kitabu hicho mwaka 1988, aliyekuwa kiongozi wa kiroho wa Iran wakati huo Ayatollah Khomeini, alimtolea Fatwa ambayo iliambatana na maagizo kwa Waislamu kumuuwa Rushdie, na watu wengine wote watakaojihusisha na kitabu hicho.

Rushdie aliishi mafichoni tangu wakati huo, lakini alianza kuonekana hadharani tangu mwaka 1998, baada ya serikali ya Iran kusema haishikilii Fatwa dhidi yake. Baadaye aliandika kitabu juu ya maisha yake ya kujifichaficha, kikiitwa Joseph Anton, jina bandia alilotumia wakati huo akiwa chini ya ulinzi wa polisi wa Uingereza.

Hata hivyo, raia wa Japan Hitoshi Igarashi aliyekitafsiri kitabu cha Rushdie, aliuawa mwaka 1991.

Pia watu wapatao 45 walipoteza maisha katika mandamano yenye ghadhabu ya kukipinga kitabu cha Rushdie, wakiwemo 12 waliokufa katika mji wake wa kuzaliwa wa Mumbai.

DW




Maofisa usalama wakimhudumia mwandishi wa fasihi Salman Rushdie, alipoanguka sakafuni baada ya kuchomwa kisu. **PICHA: DW**

# FBI yakamata nyaraka zenye siri nzito walipopekua jumba la Donald Trump

**WASHINGTON,** MAREKANI

SHIRIKA la Upelelezi wa ndani la Marekani, FBI limegundua nyaraka zenye siri nzito za serikali kutoka katika makazi binafsi ya rais wa zamani Donald Trump.

Kulingana na hati zilizochapishwa juzi na mahakama, maofisa hao wa FBI walichukua seti 11 za nyaraka wakati walipovamia na kufanya msako siku ya Jumatatu katika nyumba binafsi ya Trump ya Mar-a-Lago mjini Florida. Mbali na nyaraka zilizoainishwa kuwa siri za serikali, lakini pia kulikuwa na nyaraka ziliwekwa alama ya "siri nzito" ambazo zilikusudiwa kulinda siri muhimu za taifa na endapo zitawekwa hadharani zinaweza kusababisha athari kubwa kwa maslahi ya Marekani.

Maofisa wa FBI walikuwa wakichunguza uwezekano wa ukiukaji wa sheria tatu tofauti ikiwa ni pamoja na ile inayosimamia kukusanya, kusambaza au kupoteza taarifa za ulinzi chini ya Sheria ya Ujasusi

DW

MAKALA

# TUNAPENDA KUSIKIA YA WENZETU KULIKO YETU



Na Magabilo Masambu - 0689157789

**Wala sisemi kwamba tumefanya makosa kuupa uzito katika mijadala mitandaoni, vijiweni au kwenye vyombo vyetu vya habari kwa maana ya redio, magazeti na runinga. Kwa uzito ule ule tunapaswa kuupa hata uchaguzi wetu hapa nchini tena kwa usawa.**

TOKA Juma lililopita macho na masikio ya wana Afrika ya Mashariki pengine na maeneo mbalimbali duniani, yako Kenya kufuatilia mchakato uchaguzi unaoendelea. Sisi waandishi na vyombo vya habari tuko karibu kabisa kuhakikisha kila kitu kinachotokea huko kinajulikana kwa watu na dunia kwa ujumla jambo ambalo ni jema.

Jambo la msingi hapa ni kwamba pamoja na kuhakikisha mambo yanakuwa hadharani kwa uhuru kabisa, ni muhimu vile vile Tanzania kujifunza kuhusu namna ambavyo wenzetu wamefika mbali zaidi katika kuhakikisha wananchi wao wanapata haki ya kuhabarishwa kuhusu ucuaguzi.

Kama ambavyo tunapenda kusikia ya wenzetu, basi na sisi tunapofika katika kipindi cha uchaguzi, tupende kusikia na kuripoti kwa uwazi kama ambavyo tumeona kazi ya vyombo vyetu vya habari wakati huu.

Wakati mwingine nafikiri umekuwa utamaduni wetu kama Waafrika kwamba hata katika maisha yetu ya kila siku, huwa tunapenda kuzungumza na kusikia ya wenzetu kuliko mambo yetu. Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, katika kitabu chake cha 'Tujisahihishe', ameiita tabia hiyo kuwa tabia ya ubinafsi!

Mwalimu anasema: "Tabia moja mbaya kabisa ya binadamu ni kupenda kusema ya watu wengine kuliko ya kwake na akisema ya kwake anachagua yanayomfurahisha pekee kuliko mabaya yake."

Binafsi natambua kuwa uchaguzi wa Kenya ni muhimu kwetu kwa sababu ya ushirikiano tulio nao ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Wala sisemi kwamba tumefanya makosa kuupa uzito katika mijadala mitandaoni, vijiweni au kwenye vyombo vyetu vya habari kwa maana ya redio, magazeti na runinga. Kwa uzito ule ule tunapaswa kuupa hata uchaguzi wetu hapa nchini tena kwa usawa.

Kwa hiyo kumalizika kwa uchaguzi wa Kenya, kuendane na kujifunza mambo kadhaa ili kufanya marekebisho katika chaguzi zetu, ikizingatiwa kwamba nchini Tanzania tunatarajia kuwa na uchaguzi mkuu mwaka 2025.

Tunatarajia mijadala na kuripoti shughuli za uchaguzi zifanyike kama tulivyofanya sasa.

Jambo la pili, ni usawa katika kuwahabarisha wananchi kuhusu uchaguzi wa viongozi wao. Nimefuatilia katika uchaguzi wa Kenya na imekuwa sasa utamaduni kwamba baadhi ya wagombea hawapewi nafasi sawa na wengine katika kuripoti kampeni zao, bali ni baadhi tu ndio kila siku unawasikia kwenye vyombo vya habari.

Kenya palikuwa na wagombea wanne wa nafasi ya urais lakini taarifa za kila siku ziliwahusu wagombea wawili pekee ndiyo waliopewa nafasi zaidi katika vyombo vya habari nje na ndani na katika mijadala.

Hii haimaanishi kwamba hao wawili hawakuwa na wafuasi ambao wangependa kuwasikia.

Watu mpaka wanaaminiwa na tume ya uchaguzi, maana yake wanafaa na hawana matatizo ya akili kuwanyima nafasi ya watu kuwaona na kutowasikia na kuwanyima haki wafuasi wao na pengine hata kura chache walizozipata zimetokana na kutosikika kama wengine inawezekana kabisa kama wangelipata nafasi ya kusikiwa na watu wangepata kura nyingi zaidi.

Tumeshuhudia hapa nchini mwendo ule ule kwamba baadhi ya wagombea wanapata nafasi zaidi kwenye vyombo vya habari kuliko wengine.

Ni kasoro inayohitaji marekebisho makubwa na ya haraka kwa sababu vyombo vya habari kufanya hivyo tutakuwa tayari vinakuwa vimeshawachagulia wananchi mwelekeo kabla ya uchaguzi wenyewe.

Kazi yetu kama waandishi nadhani ni kumwonyesha kila mtu kazi ya kuchagua ibaki kwa wananchi.

Pengine niamini kwamba inawezekana kunakuwa na maelekezo kwa sababu sidhani kama maadili ya kiuandishi yanaruhusu lakini si maadili tu bali tunakuwa tunavunja katiba zetu. Moja, kuleta ubaguzi ambao umepigwa marufuku na katiba.

Pili, baadhi ya watu wanakuwa wamenyimwa uhuru wa kupata habari kutoka kwa watu ambao wangewatarajia badala yake wanalazimishwa kuwasikia wasiyowapenda.

Uchaguzi huu wa Kenya utufundishe mengi. Si kujifunza tu bali tuyatekeleze kwa vitendo. Jambo jema kabisa tukapata nafasi ya pekee ya kumpata mwenyekiti ya waangalizi wa uchaguzi Afrika mashariki Jakaya Kikwete, ambaye sina shaka naye kuhusu masuala ya diplomasia ya hali ya juu kabisa, nikasikia siku moja anasema wale watakaokuwa wameshindwa kwenye uchaguzi huo wa rais waende mahakamani.

Je, hapa kwetu sheria za uchaguzi zinasema nini kuhusu mtu aliyeshindwa katika nafasi ya urais na ana malalamiko? Tuna jambo la kujifunza hapo

Ni imani yangu kwamba, uchaguzi huu utatufanya tuwe na uchaguzi bora kabisa wenye kuigwa mwaka 2025 kuanzia kwenye vyombo vya habari kuripoti kwa uwazi na kwa usawa ili kuwapa nafasi wananchi kumpima mgombea mmoja mmoja na mwisho waamuwe wenyewe na uamuzi huo uheshimiwe na tume yenye mamlaka ya kusimamia uchaguzi huo.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Mbaraka alipoonya kuingilia ugomvi kati ya mtu na mkewe*



Na Adam Fungamwango

NAKUMBUKA zamani kuna mama mmoja aligombana na mumewe, akaamua kukusanya kilicho chake ili aondoke. Akamwita dada wa chumba cha pili aje kumsadia kukusanya vile vyote ambavyo alikuwa anahitaji.

Yule dada alikubali, lakini wenzake walimkataza, wakamwambia amwache mwenyewe afanye kazi hiyo. Lakini ni kama yule dada ambaye ni shoga yake kipenzi aliamua kuwa na upande. Akawa yuko upande wa shoga yake, akimsaidia rafiki yake huku akiungana naye kumshutumu mwanaume kwa kutomtendea haki mkewe. Mke akaondoka, yule dada akabaki hapo hapo na wenzake. Mume naye akabaki peke yake.

Hiyo ilikuwa nyumba yenye wapangaji wengi. Mwezi mmoja tu ulipita. Mke akarudi kwa mumewe. Sijui ilikuwaje? Kama mume alienda kubembeleza au mke aliomba msamaha lakini kilichoonekana kwa watu ni kwamba walikuwa wote na wakaendelea kuishi kama zamani.

Cha ajabu ni kwamba yule dada ambaye alimsaidia shoga yake kuchukua vitu ndani na kumzodoa mume sasa ananuniwa na wote wawili. Kwa mume sawa, lakini mke ambaye alimsaidia ilikuwa inashangaza kidogo. Tena yeye ndiye akawa adui yake kabisa. Akawa anawaambia watu kuwa ndiye aliyeleta ugomvi huo wa yeye na mumewe kukosana. Pia ikaenda mbali zaidi, mke akadai kuwa shoga yake alitaka aondoke ili yeye aingie ndani kama mke.

Mara nyingi mambo ya ugomvi wa mke na mume yana mambo mengi sana. Ndiyo maana wazee wa zamani wanasema ugomvi wa mtu na mpenzi wake au mumewe usiuingilie.

Wanajua kuna jambo dogo tu linalosababisha hilo ambalo kwa wakati huo halijarekebishika lakini dosari zikiondolewa, wataendelea kupatana na walioingilia watabaki na aibu.

Wanaposema usiingilie, si kama wakipigana watu usiamue, au wanapopeleka kesi kwa wakubwa wakiiamua, la hasha. Wanaposema usiingilie, wana maana kuwa upande mmoja kati ya hao wawili. Yaani unamsaidia mume kumshutumu mke, au unakuwa upande wa mke kumuona mume amekosea.

Hili ni kosa kubwa sana. Kinachotakiwa ni kuwaamulia na kuwataka waache mzozo, kutupiana maneno, kupigana, au mmoja kumpiga mwingine.

Mfano mwingine kuna mwanamke alikuwa anaumwa huko Kisemvule pembezoni mwa Dar es Salaam. Mume wake akawa hamjali hata kumpeleka hospitalini akashindwa. Mke kwa hasira akawapigia simu ndugu zake, ambao walikwenda huko kwa hasira na kumtukana sana mwanamume. Wakamchukua ndugu yao na kumpeleka Kunduchi kwa mmoja wa ndugu, akatibiwa.

Kabla hata hajapona vizuri, mke akatoroka na dawa zake kurudi kwa mumewe. Kumbe siku zote walikuwa wakiongea kwa simu na kuyajenga. Ndugu waliomtibia na kumtukana jamaa wakabaki midomo wazi.

Ndiyo maana mwanamuziki Mbaraka Mwinshehe aliwahi kutunga wimbo akauita 'Ugomvi Mke na Mume'. Alionya kabisa kuingilia ugomvi wao kwani baadaye watu wanaweza kupata lawama. Haya ndiyo mashairi ya wimbo huo yenye mafunzo makubwa kwenye jamii.

"Wanapogombana ooo, mtu na mke wake ndani ya nyumba, usiingilie kati kabisa ugomvi wao. Utakuja pata balaa we kijana, ya kusingiziwa mengi na isitoshe, leo unagombombelezea mwisho wake utapata lawama.

"Hayo yashike kichwani, usijitie kimbelembele, usipoelewa neno lolote usijitie wajua. Wengine hawana masihara, hata hasira hazijamuisha wewe wamtibua, hatari wajitakia ooo. Kinachokuuma kitu gani, ugomvi yeye na mke wake, waingilia kwa nini, waitafuta lawama. Hatari wajitakia, waitafuta lawama. Ugomvi yeye na mke wake, waingilia kwa nini? Ukipigwa panga mbele ya hakimu utasemaje?"

Haya ni mashairi ya wimbo huo uliotungwa na kupigwa na mwanamuziki huyo miaka ya 1970 ambao maudhui yake hadi leo yanaishi. Hii ndiyo tofauti ya tungo za zamani na za sasa. Tungo za sasa pamoja na kwamba nyingi ni za mapenzi, lakini ni za kufikirika zaidi.

Unapotungwa wimbo uliomhusu mtu fulani, au kitu fulani cha kijamii hata kama kilitokea miaka ya 1910, lakini kwa sasa unaihusu jamii, basi maudhui yake yataendelea kuishi kwa sababu maisha yanaendelea kuwa ni yale yale.

Watu wanazaliwa, wanakua, wanaoa, wanaolewa, wanazaa na hatimaye wanakufa. Kwenye maisha kuna vitu vingi ambavyo vinafanana kwa asili ya binadamu.

Kilichompata mtu wa miaka hiyo, ni lazima kimpate wa miaka hii. Hakuna kipya zaidi duniani, yote yanajirudia tu. Matatizo ya ndoa, kuachwa, kutorokwa, kuachana, roho za kwa nini, mgogoro wa wake na mawifi, yote yalianza karne na karne na hadi leo yanaendelea na yataendelea kuwepo. Ndiyo maana wanamuziki wanaotunga nyimbo kwenye maeneo haya, zinaendelea kuishi na kufundisha, licha ya kwamba wengi wao wameshafariki dunia.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na walipomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-14

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

HE, kumbe wewe, umefika, yaani nilikuwa mbali sana." Akajibu akiwa amesimama karibu naye, jambo ambalo lilimfariji na kumpeleka mbali Prince.

"Yaani jana tu umeanza kunisahau Hasnat?" Akauliza kwa utani.

"Mmh, mwenzangu ulivyokuja jana siyo kama leo. Angalia leo ulivyotokelezea, na ndevu zako zile za jana umenyoa." Akajibu Hasnat kwa sauti ya chini ili asisikie mtu, lakini ikiwa laini kama sufi.

Prince aliangua kicheko. "Nimesema kuna mzigo mwingine humu ndani ya gari, ngoja nikupe kabisa uwe na mizigo miwili. Akatoa mfuko ambao ulikuwa na nyama, samaki, sukari na mafuta ya kupikia ambayo yalikuwa nyumbani kwao anakoishi na baba yake.

"Huo wako, lete nikusaidie mimi." Wakaingia kwenye mlango mkubwa wa bati. Hidaya alikuwa amekaa kwenye kizingiti cha nyumba "Karibuni." Akanyanyuka na kwenda kumpokea Prince mzigo, huku akimuacha Hasnat akiwa na mzigo wake wakaingia ndani.

"Karibu mwanangu." Akakaribisha tena.

"Ahsante mama." Akaitikia baada ya kukaa kwenye kochi. Sehemu ni ile ile ambayo alikaa jana usiku.

Hidaya na binti yake walishangazwa na mgeni wao alivyokuja leo ni tofauti na jana usiku. Walikuwa kama watu wawili tofauti. Wa jana aliingia akiwa mbabe, katili aliyejaa vitisho, ingawa baadaye akawa mpole ghafla.

Huyu wa leo ni mstaarabu sana, aliyevaa nguo za ujana, lakini za heshima, akitembea na kuongea kistaarabu, mwenye tabasamu na furaha tele.

Hata muonekano ulikuwa tofauti. Prince alilijua hilo, ndiyo maana alinyoa ndevu zake zilizoanza kuota na yeye kuziachia, lakini alichagua nguo ambazo za ujana sana.

Hata ule wasiwasi tena hawakuwa nao. Hawakuona hata chembe ya maigizo kwenye uso wake. Alionekana kubadilika kabisa, hivyo nao kama alivyogundua hilo jana yake, walimpokea vizuri bila wasiwasi wowote.




**"Hata mimi sikutegemea sana, tulisema hadi ikifika saa tano hajaja, basi tunywe, halafu tumbakishie kama akija sawa, asipokuja basi." Hidaya aliendelea kuongea na Prince.**

"Karibu mwanangu, unajua hata chai sisi hatujanywa, tulikuwa tunakusubiri wewe. Wakati tunapika, Hasnat akasema mama tusinywe tumsubiri mgeni wetu kama akija tunywe naye."

"Alijua siwezi kuja?"

"Hata mimi sikutegemea sana, tulisema hadi ikifika saa tano hajaja, basi tunywe, halafu tumbakishie kama akija sawa, asipokuja basi." Hidaya aliendelea kuongea na Prince.

Haikuwa chai ambayo ameizoea sana ile ya maziwa, mayai, slesi za mikate, badala yake ilikuwa ya rangi, vitumbua pamoja na kiporo cha wali, maharage na kisamvu cha jana.

Prince hakuzoea, lakini alifurahia chakula hicho. Kwa mara ya kwanza alikuwa anakula chakula na watu wengi kwa pamoja. Alijisikia amani na furaha ambayo hakuwahi kuwa nayo. Aligundua kwa kumbe kuna vitu vizuri duniani alichelewa kuvitambua, ikiwemo kujumuika na watu, pamoja na baadhi ya vyakula vya uswahilini.

"Hivi mama, Hasnat huyu ni wa ngapi?" Prince akauliza kiutani. Lilimtoka ghafla tu kwa ajili ya kuanzisha mazungumzo, kwani kila mmoja hakujua aanze na nini.

"Mhh, we mwanangu acha tu. Ni huyo huyo mmoja tu, kwanza na wa mwisho na haiwezekani tena mimi kupata mtoto."

"He, kwa nini?"

"Ni habari ndefu, lakini nitakuhadithia kwa ufupi. Wakati nikiwa msichana nilikuwa nikifanya kazi za ndani. Nilikuwa mdada wa kazi, nilipoachia, nikapata kijana mmoja akanipenda nikakaa naye, baada ya kupata ujauzito akanifukuza nyumbani kwake. Nikawa mtu wa kutangatanga, mjini hapa ndugu sina, nikahifadhiwa na mama mmoja hadi nilipojifungua huyu Hasnat."

Wakati anahadithia hayo, binti mwenyewe alikuwa amekaa kinyonge amejikunyata kwenye kochi akisikiliza stori ya mama yake.

"Baada ya hapo nikaanza kuhangaika huko na huku, nikaanza kufanya biashara mbalimbali, kuuza maji, mihogo, karanga, kucheza vikoba, mpaka nikaanza kuwa mama lishe. Mpaka leo hii ndiyo kazi yangu, imeniwezesha kujenga hivi nyumba viwili naishi na binti yangu, amemaliza chuo hivi karibu mwenzio huyo."

"Pole sana mama." Prince alimpa pole akimpa mkono.

Hidaya naye alipeleka mkono wake kwa Prince, lakini kama kuna kitu alikuwa akikiangalia kwa makini.

"Ahsante sana mwanangu." Akaitikia, lakini kwa hali ambayo haikuwa ya kawaida.

Akamtazama tena kwa makini usoni kiasi cha hata Prince mwenyewe akashangaa.

"Mhh, mbona kama..., wewe siyo Prince?" Hidaya akauliza na kuwashtua wote waliokuwa ndani.

Prince na Hasnat walipigwa na mshangao kuona mama ameuliza kama mtu anayemfahamu.

Prince akashangaa zaidi kwani hakutegemea mama yule ambaye jana yake kama alivyopanga saa hizi angekuwa marehemu, leo anamtaja kwa jina.

"Unanifahamu?" Akauliza kwa mshangao.

"Nauliza wewe ndiyo Prince au?"

"Ndiyo mimi."

Hidaya aliruka pale alipokuwa na kumkumbatia mama anavyomkumbatia mtoto wake mchanga.

"Aaah, mwanangu, kumbe upo hai? Umekuwa mkubwa baba." Haya yote yaliyokuwa yanafanyika yalikuwa ni kama ndoto kwake. Kila kitu alichokiona kuanzia jana hadi leo ilikuwa ni kama anaangalia filamu moja ya ajabu ambayo hajawahi kuishuhudia kwenye maisha yake.

"Jana nilitaka kumuua, nikampenda binti yake, nimekuja leo kwa ajili ya kuunganika na familia hii, leo niliyetaka kumuua, ninayetarajia awe mkwe wangu, anaonekana kunifahamu, ananiita mwanagu. Kwa nini?"

"Kumbe ulitaka kuniua mama yako." Hidaya aliongeza huku akianza kuangua kilio.

Hasnat alitaka kumbembeleza mama yake. Prince akamzuia. "Mwache kwanza, kuna kitu hapa si cha kawaida."

Hata Hasnat aliamini hivyo. Akajiuliza kwa nini tangu jana hakumtambua, na hadi leo hakuweza kumtambua hadi walipopeana mikono.

Dakika tano zilipita. Hidaya akanyamaza na kuanza kujifuta machozi.

"Mama uko sawa?" Hasnat alimuuliza.

"Niko sawa mwanangu, ila nimeumia sana."

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# Nandy, Mwijaku wapotezeana

URAFIKI kati ya mwanamuziki maarufu wa kike, Faustina Mfinanga, maarufu kama Nandy na Mtangazaji wa Clouds FM, Burton Mwambe, anayejulikana kwa jina la Mwijaku, umefikia ukingoni baada ya wawili hao kuburuzana mahakamani.

Wawili hao kama vile hawajuani wanapokutana katika mahakama ya mwanzo ya Sinza jijini Dar es Salaam, ambako imefunguliwa kesi ya madai.

Mwijaku anadai kuwa alitumiwa vibaya na Nandy pasina makubaliano yake.

Anadai walielewana na Nandy afanye tangazo kwa ajili ya Nandy Festival, lakini alipomaliza kulitengeneza Nandy alilikataa. Hata hivyo alishtukia tangazo hilo ameliweka kwenye mtandao wa kijamii na alishindwa kuelewa.

Kesi hiyo imeahirishwa mpaka tarehe 19-8-2022, kwa wahusika kuwasilisha nyaraka stahiki ikiwamo mkataba waliokubaliana.

Baada ya kutoka mahakamani hapo, kila mtu alionekana kuelekea upande wake huku Nandy akishindwa kuongea na waandishi kama ilivyo kawaida yake.

# Mobetto mbona unawapa maswali?

MWANAMITINDO na mwanamuziki wa Bongo Fleva, Hamisa Mobetto, ametikisa tena katika mitandao ya kijamii baada ya kuonyesha tukio la kukabidhiwa gari jipya na mpenzi wake.

Mobetto alipewa gari hilo aina ya Range Rover, na mpenzi wake huyo katika tukio la kushtukiza akiwa katika hoteli ya kifahari na marafiki zake.

Hata hivyo, baadhi ya watu walimuandama kwa kumwambia tukio hilo litakuwa limepangwa kwani mazingira yote yalionekana kuna vitu vimefichwa na kuratibiwa ili kuonekana ni kweli amepewa zawadi.



HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ZIYECH AWANIWA MAN

KLABU ya Manchester United inataka kumsajili winga wa zamani wa Chelsea kutoka Morocco, Hakim Ziyech, 29, baada ya kushindwa kukabiliana na ushindani wa mshambuliaji Mjerumani, Timo Werner ambaye amehama kutoka Chelsea kwenda RB Leipzig. ***(Manchester Evening News)***

### PULISIC AWINDWA

KLABU ya Newcastle United inaweza kumlenga mshambuliaji wa Chelsea, Mmarekani Christian Pulisic, 23. ***(The Athletic, via Mail)***

### DEPAY ATAKIWA WEST HAM

WEST Ham wamewasilisha fedha nyingi za ofa kwa Barcelona kwa ajili ya mshambuliaji Mholanzi, Memphis Depay, 28. ***(Football Insider)***

### UI-JO KUTUA FOREST

KLABU ya Bordeaux imekubali ofa ya euro milioni 4 kutoka kwa klabu ya Nottingham Forest kwa ajili ya mshambuliaji wa Korea Kusini, Hwang Ui-jo, 29. ***(L'Equipe)***

### NDOMBELE KWA MKOPO

KLABU ya Napoli imefikia makubaliano na Tottenham Hotspur ya kumsajili kwa mkopo, Mfaransa Tanguy Ndombele, 25, huku kukiwa na chaguo la kumnunua. ***(Fabrizio Romano)***

### WILLIAN HUYO FULHAM

MPANGO wa Willian, 34, wa kuhamia katika Klabu ya Fulham umefikia katika hatua ya mwisho baada ya winga huyo wa Brazil kuvunja mkataba na Corinthians. ***(Nicola Schira)***

### DIENG AWANIWA

KLABU ya Fulham imejiunga na mbio za kuisaka saini ya mshambuliaji Msenegal, Bamba Dieng, 22, kutoka Marseille, huku Celtic pia wakimtaka. ***(90min)***

### BELLERIN KWENDA BARCELONA

MLINZI wa kulia wa Hispania, Hector Bellerin, 27, amepewa ofa ya kwenda Barcelona wakati mchezaji huyo akijadiliana kuhusu kusitisha mkataba wake na Arsenal.***(Mail)***

### DEST ATAKIWA MAN

BARCELONA wanafanya mazungumzo na Manchester United kuhusu kumuuza beki wa pembeni wa Marekani, Sergino Dest, 21, huku klabu hiyo ya Hispania ikitaka ada ya euro milioni 20. ***(AS)***

### MAN YASAKA KIPA

MANCHESTER United wanaendelea kutafuta mlinda mlango atakayesaidiana na David de Gea, huku kipa wa zamani wa Southampton, Alex McCarthy, 32, akiwa kwenye rada zao. ***(Mali)***

### GOMEZ WA MWISHO CITY

KOCHA Pep Guardiola anatarajia Sergio Gomez, 21, kuwa mchezaji wa mwisho kusajiliwa Manchester City msimu wa joto, huku beki huyo wa Hispania akikaribia kukamilisha uhamisho kutoka Anderlecht. ***(Sun)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI HAYUPO TUZO YA BALLON D'OR 2022

**Ni kwa mara ya kwanza baada ya miaka 17, Ronado ajumuishwa na...**

**PARIS,** Ufaransa

LIONEL Messi ameachwa nje ya tuzo ya Ballon d'Or kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2005, na mshindi huyo wa zamani mara saba hajateuliwa kuwania tuzo hiyo ya 2022.

**Orodha ya wanaowania 2022, iliyofichuliwa na jarida la France Football Ijumaa, ilikuwa na majina 30, lakini Messi ambaye anaichezea Paris Saint-Germain hakujumuishwa.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 aliondoka Barcelona na kujiunga na PSG msimu uliopita wa joto wakati miamba hiyo ya Katalunya iliposhindwa kusajili mkataba wake mpya waliokubaliwa kwa sababu ya matatizo ya kifedha.

Ingawa bado alikuwa na asisti nyingi, alifunga mabao 11 pekee katika mashindano yote - na mabao sita pekee kwenye Ligue 1.

Baada ya misimu 13 mfululizo ya kufunga angalau mabao 30 akiwa na Barcelona, ilikuwa ni hesabu ya chini kabisa ya mabao ya Messi kwa msimu mmoja tangu 2005/06, ambao ulikuwa msimu wake wa kwanza kamili akiwa na kikosi cha kwanza cha Barca.

Ukiondoa mwaka 2020 ambapo hakukuwa na tuzo kwa sababu ya janga la Covid-19, Ballon d'Or pekee zaidi ya 2022 ambayo Messi hajateuliwa ni 2005 wakati alikuwa hajatimiza umri wa miaka 18.

Messi anabakia kuwa mshindi wa rekodi ya tuzo ya Ballon d'Or akiwa ameshinda mara saba. Ameshinda mwaka 2009, 2010, 2011, 2012, 2015, 2019 na 2021.

Mpinzani wa muda mrefu Cristiano Ronaldo, ambaye ameteuliwa mwaka huu 2022, ameshinda mara tano.

SportPesa LIVE IN PLAY

MECHI KALI
CHELSEA
VERSUS
TOTTENHAM
1 | 2.24
X | 3.26
2 | 3.06

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TEN HAG: RONALDO HAJAZUNGUMZA NA MIMI



**MANCHESTER,** England


KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag amedai kuwa Cristiano Ronaldo hajazungumza naye kuhusu kutaka kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto.

Ronaldo alielezea nia yake ya kuondoka United kutafuta timu inayocheza Ligi ya Mabingwa Ulaya mapema msimu huu wa joto na alikosa mechi za kujiandaa na msimu mpya kwa 'sababu za kibinafsi', na ameanza maisha polepole chini ya bosi huyo mpya, ambaye alihisi fowadi huyo hakuwa fiti vya kutosha na alihamia benchi wakati United ikifungwa na Brighton.

Huku kukiwa na hali ya sintofahamu, Ten Hag amesisitiza mara kwa mara nia yake ya kutaka kumuweka Ronaldo karibu, akitaka kumfanya aongeze kasi ili kupata nafasi ya kucheza.

"Ronaldo akitaka kuondoka ni mawazo yake. Hilo mimi hajaniambia," alisema Ten Hag.

"Kwahiyo nashughulika na wachezaji tulionao na tunapanga naye kwa ajili ya msimu huu na tumefurahishwa naye na tunatakiwa kumuweka sawa kwenye timu hivyo anatakiwa kuja katika viwango sahihi vya utimamu wa mwili ili aweze kufanya kazi hiyo. ambayo tunatarajia afanye.



## *Barca yasajili wapya kasoro Kounde*

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imesajili wachezaji wake wote wapya kwenye mfumo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, isipokuwa Jules Kounde kabla ya mchezo wao wa ufunguzi wa jana Jumamosi dhidi ya Rayo Vallecano.

Klabu hiyo ya Katalunya imefanya usajili mkubwa msimu huu wa joto ili kushindana na Real Madrid kwenye Ligi na Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakitumia karibu euro milioni 150 kuwanunua Robert Lewandowski, Raphinha na Kounde.

Barca pia ilifanikiwa kuwasajili Andreas Christensen na Franck Kessie kwa uhamisho wa bure, pamoja na kuwapa mikataba mipya Ousmane Dembele na Sergi Roberto.

Matatizo makubwa ya kifedha yaliizuia klabu hiyo kusajili mikataba hiyo mipya kwa sababu ya kanuni ya matumizi ya fedha za La Liga.

Hali kama hiyo msimu uliopita wa joto ilisababisha Lionel Messi kuondoka klabuni hapo kwa sababu hawakuweza kumudu mkataba wake kwa sababu ya mshahara wake mkubwa.

Barca wametumia majira ya joto kutafuta fedha za ziada na mapato ambayo yangewawezesha kusajili rasmi wachezaji wao wapya na mikataba na La Liga.

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA

# MCHENGERWA ATOA MAAGIZO, MASHUJAA MADOLA WAZAWADIWA

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa ameliagiza Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) kupitia upya kanuni kwa kuwashirikisha wadau wote wa Sanaa nchini Tanzania ili ziweze kuainisha bayana mfumo mzuri wa ufanyaji kazi unaowashirikisha wasanii binafsi, vyama, na mashirikisho ya Sanaa.

Mchengerwa ameyasema hayo usiku wa kuamkia jana katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Mwl Julius Nyerere jijini Dar es Salaam baada ya kupokea taarifa rasmi ya namna bora ya ya kusimamia HAKIMILIKI na Mirabaha kwa wasanii nchini kutoka kwa Kamati aliyoiteua Julai Mosi mwaka huu iliyoongozwa na Victor Tesha.

"Mfumo huu utasaidia kuwatambua wasanii wote nchini na kuweza kuwahudumia kwa urahisi kwani mfumo uliopo sasa unatoa nafasi ya kila msanii kujitafutia riziki mwenyewe kitu kinachofanya wasanii wengi kukosa umoja na kuzalisha migogoro isiyokuwa na tija," alisema Mchengerwa.

**Pia, ameliagiza BASATA kufanya mapitio na usuluhishi katika migogoro ya wasanii, ikiwa ni pamoja na kuandaa dawati la ushauri wa kisheria kuhusu Mikataba na masuala ya Sanaa.**

Mchengerwa pia alikabidhi bonus ya Tsh. 30,000,000 itakayogawanywa kwa wachezaji na benchi la ufundi lote lililoshiriki katika michezo ya Jumuiya ya Madola pamoja na kuwapatia fedha wachezaji watatu walioshinda medali kwenye mashindano hayo.

Wachezaji hao ni Nahodha wa timu ya Tanzania, Felix Simbu aliyetwaa medali ya fedha na kunyakua dola 7500 na Mabondia, Yusufu Changalawe na Kassim Mbundwike waliotwaa medali za shaba ambao Serikali iliwapatia dola za kimarekani 5000 kila mmoja.

Katika kuhakikisha timu za Tanzania zinaendelea kufanya vizuri kwenye mashindano ya kimataifa Mchengerwa ameielekeza Idara ya Michezo na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kuanza maandalizi haraka ya kuandaa Timu za Taifa kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya ALL AFRICAN GAMES yatakayofanyika nchini Ghana katika mji wa Accra kuanzia Agosti 14 hadi 18 mwaka 2023.




Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa (katikati), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya dola 7,000, kwa mwanariadha, Alphonce Simbu (wa pili kulia), kwa kushika nafasi ya pili katika mashindano ya Jumuiya ya Madola yaliyofanyika nchini England wakati wa hafla ya kuwapongeza wachezaji wa Tanzania iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Taa za Mkwakwani kutoathiri Ligi Kuu*

**Na Cheji Bakari, TANGA**

MENEJA wa uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, Nassoro Makau amesema kuwa shughuli ya usimikaji wa miundombinu ya taa inayoendelea katika uwanja huo haitaathiri mechi za Ligi Kuu Bara.

Ligi Kuu Bara inatarajiwa kuanza kutimua vumbi Agosti 15 mwaka huu na kwa upande wa Tanga, Coastal Union itafungua pazia la ligi hiyo Agosti 17 kwa kuikaribisha timu ya KMC.

Amefafanua kuwa shughuli zinazoendelea hapo haziwezi kuingiliana na suala lolote la kimichezo linaloendelea ndani ya uwanja huo.

"Miundombinu ya ufungaji wa taa hizo inafanyika nje ya uwanja hivyo mashabiki wasiwe na wasiwasi mambo yote yataenda sambamba bila kuathirika kwa upande wowote," alisema Makau.

Zoezi hilo la ufungaji wa taa ambalo linafanywa na kampuni ya Azam Media Limited ambao wana hisa ya asilimia 75 kwa kushirikiana na uongozi wa uwanja wa Mkwakwani ambao wana hisa ya asilimia 25 lilianza mwishoni mwa wiki iliyopita na linatarajiwa kukamilika baada ya wiki tatu.

Hatua iliyofikia hadi sasa ni uchimbaji wa mashimo ya kusimika miundombinu kuzunguka uwanja ambapo kukamilika kwa zoezi hilo kutaufanya uwanja huo kuwa na uwezo wa kuchezwa mechi za usiku.

SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAPILI - 14/08/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 2193 | FC Volendam vs NEC Nijmegen | 2.50 | 3.49 | 2.55 |
| 14:00 | 1427 | Lorient vs Lyon | 4.11 | 3.81 | 1.76 |
| 14:00 | 4436 | Kilmarnock vs Celtic | 12.98 | 6.39 | 1.19 |
| 14:30 | 5762 | St Truiden vs Anderlecht | 3.56 | 3.41 | 2.00 |
| 15:00 | 3710 | FK Khimki vs Akhmat Grozny | 2.49 | 3.19 | 2.74 |
| 15:00 | 5467 | Viborg FF vs Silkeborg | 2.91 | 3.41 | 2.28 |
| 15:15 | 3978 | FC Winterthur vs FC Zurich | 2.81 | 3.51 | 2.30 |
| 15:30 | 4663 | Twente vs Fortuna Sittard | 1.46 | 4.50 | 5.80 |
| 15:30 | 5796 | Ajax vs Groningen | 1.15 | 7.41 | 13.02 |
| 16:00 | 1523 | Middlesbrough vs Sheffield Utd | 2.43 | 3.21 | 2.81 |
| 16:00 | 1923 | Malmo vs GIF Sundsvall | 1.14 | 7.06 | 12.74 |
| 16:00 | 3085 | Reims vs Clermont Foot | 2.14 | 3.22 | 3.37 |
| 16:00 | 3572 | AC Ajaccio vs Lens | 3.07 | 3.17 | 2.30 |
| 16:00 | 3774 | Troyes vs Toulouse | 2.61 | 3.16 | 2.66 |
| 16:00 | 3787 | AJ Auxerre vs Angers | 2.17 | 3.26 | 3.26 |
| 16:00 | 3927 | AIK Football vs IFK Varnamo | 1.55 | 3.77 | 5.29 |
| 16:00 | 5576 | Djurgardens IF vs Kalmar | 1.54 | 3.84 | 5.31 |
| 16:00 | 5737 | Nottingham vs West Ham | 4.00 | 3.50 | 1.84 |
| 16:30 | 5210 | Mainz vs Union Berlin | 2.23 | 3.19 | 3.14 |
| 17:00 | 2386 | Baumit Jablonec vs Slavia Prague | 4.99 | 3.72 | 1.69 |
| 17:00 | 3093 | Eupen vs Royal Antwerp | 3.73 | 3.63 | 1.88 |
| 17:00 | 4034 | Hearts vs Dundee Utd | 1.58 | 3.76 | 5.62 |
| 17:00 | 4677 | Blackburn vs West Bromwich | 2.67 | 3.17 | 2.57 |
| 17:30 | 4134 | FC Basel vs FC Lugano | 1.82 | 3.73 | 3.88 |
| 17:30 | 4565 | BSC Young Boys vs Servette Geneva | 1.54 | 4.42 | 5.03 |
| 17:30 | 5425 | Boavista vs Santa Clara | 2.50 | 3.07 | 2.86 |
| 17:45 | 3524 | Sparta Rotterdam vs AZ Alkmaar | 3.95 | 3.45 | 1.86 |
| 18:00 | 3733 | LASK Linz vs Rapid Vienna | 1.77 | 3.59 | 3.89 |
| 18:00 | 5252 | Austria Lustenau vs TSV Hartberg | 2.26 | 3.33 | 2.79 |
| 18:00 | 5388 | RB Salzburg vs Wolfsberger AC | 1.21 | 5.90 | 9.64 |
| 18:05 | 5205 | Nice vs Strasbourg | 2.15 | 3.21 | 3.36 |
| 18:30 | 3219 | Cadiz CF vs Real Sociedad | 3.38 | 3.18 | 2.18 |
| 18:30 | 4225 | Chelsea vs Tottenham | 2.24 | 3.26 | 3.06 |
| 18:30 | 4820 | Bayern Munchen vs VfL Wolfsburg | 1.12 | 8.39 | 14.98 |
| 19:00 | 2200 | Brondby vs Odense | 1.87 | 3.53 | 3.88 |
| 19:15 | 2091 | Umraniyespor vs Antalyaspor | 3.02 | 3.28 | 2.28 |
| 19:30 | 3544 | Lazio vs Bologna | 1.54 | 4.20 | 5.20 |
| 19:30 | 4870 | Fiorentina vs Cremonese | 1.38 | 4.70 | 7.00 |
| 19:30 | 4964 | OH Leuven vs Brugge | 4.43 | 3.93 | 1.68 |
| 20:00 | 4991 | Sparta Prague vs Sigma Olomouc | 1.38 | 4.89 | 7.75 |
| 20:00 | 5710 | Spartak Moscow vs Sochi | 1.97 | 3.54 | 3.44 |
| 20:00 | 5831 | FC Vizela vs Porto | 9.62 | 5.41 | 1.27 |
| 20:30 | 2320 | Valencia vs Girona | 1.85 | 3.45 | 4.16 |
| 21:45 | 1165 | Brest vs Marseille | 3.93 | 3.68 | 1.82 |
| 21:45 | 3186 | Alanyaspor vs Besiktas | 2.80 | 3.50 | 2.31 |
| 21:45 | 3573 | Spezia vs Empoli | 2.41 | 3.25 | 2.80 |
| 21:45 | 4962 | Salernitana vs Roma | 6.19 | 4.30 | 1.46 |
| 22:00 | 4971 | Zulte Waregem vs Racing Genk | 4.01 | 3.91 | 1.75 |
| 22:30 | 2240 | Vitoria Guimaraes vs GD Estoril | 2.03 | 3.31 | 3.57 |
| 23:00 | 4239 | Almeria vs Real Madrid | 6.48 | 4.76 | 1.42 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumapili Agosti 14, 2022

Nipashe



Messi hayupo Ballon d'Or 2022

UKURASA 21

# Tulisema tutawachapa

Saada Akida na Adam Fungamwango

## ● ● ● Mayele apeleka msiba Msimbazi, aitungua Simba kwa mara ya pili Ngao ya Jamii Yanga ikibeba tena..



Wachezaji wa Yanga wakishangilia moja kati ya mabao yao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

NI yule yule Fiston Mayele aliyefunga bao pekee kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa mwaka jana katika mechi ya Ngao ya Jamii, Septemba 25, jana aliiua tena Simba akifunga mabao mawili yaliyoipa tena Yanga ushindi kwa mara ya pili mfululizo.

Kwenye mechi hiyo ya watani wa jadi iliyokuwa maalum kwa ufunguzi wa Ligi Kuu msimu wa 2022/23, Simba ilitawala zaidi kipindi cha kwanza na Yanga kuwakimbiza wapinzani wao kipindi cha pili, lakini hadi mwisho mshindi wa ngao msimu uliopita akatoka uwanjani na mabao 2-1.

**Ilioneka kabisa kuwa bado Simba ina tatizo kubwa kwenye eneo lake la viungo wakabaji, kwani wachezaji wa Yanga wakiamua kuondoka, basi wanawafikia kwa urahisi mabeki wa Simba, au kipa wao Beno Kakolanya.**

Ni eneo ambalo linaonekana sugu na halijapatiwa majibu kwenye kikosi cha Simba, kwani pamoja na kuonekana dhahiri msimu uliopita, hata kwenye mechi ya Simba Day dhidi ya St George lilionekana pia.

Na kama si uhodari wa kipa Kakolanya aliyeokoa mabao yapatayo matatu ya wazi kutoka kwa mastraika wa Yanga, Stephane Aziz Ki na Mayele, basi Simba ingeoga mabao mengi.

Pia beki Mohamed Outtara alifanya kazi kubwa kwenye mechi ya jana, akishirikiana na Henock Inonga, lakini hawakuwa na watu wa mbele wazuri wa kuwalinda.

Simba ilianza kupata bao dakika ya 15 kupitia kwa mchezaji wa kimataifa wa Senegal, Pape Sakho alipoiandikia Simba bao la kuongoza, baada ya pasi ndefu ya Chama kutoka winga ya kushoto kukatiza mpaka winga ya kulia, huku mabeki wa Yanga wakiwa wamesimama kutengeneza mtego wa kuotea, kiungo huyo alitoka nyuma na kuunganisha mpira bila kutuliza, ukimpita kipa Diarra na kukwama wavuni.

Aziz Ki, nusura aisawazishie Yanga dakika ya 23, kama si uhodari wa kipa Kakolanya kuruka na kuliwahi shuti lililopigwa na kiungo huyo ambalo lilikuwa likielekea wavuni.

Hiyo ilitokana na nona fupi iliyopigwa na wachezaji wa timu hiyo na kumpa kiungo huyo aliyesajiliwa msimu huu akitokea Asec Mimosas.

Diarra aliiokoa Yanga kufungwa bao la pili dakika ya 38, alipodaka kwa ustadi mpira wa kichwa uliopigwa na Sadio Kanoute, kutokana na mpira wa faulo uliopigwa na Sakho.

Mabadiliko yaliyofanywa kipindi cha pili kwa timu zote kwa kiasi kikubwa yaliisaidia Yanga, kwani iliamua kupita kati baada ya kocha Nasreddine Nabi kugundua udhaifu kwenye nafasi ya kiungo mkabaji wa Simba, akimhamisha Aziz Ki kutoka pembeni na kumuingiza kati, akawa na kazi ya kuchukua mipira na kuanza kutembea kati akiwa hakabwi na wakati anafikiwa na mabeki wa Simba, anagawa mpira kwa Mayele au Bernard Morrison ambao walikuwa wanatengeneza hatari kubwa kwenye lango ya wapinzani.

Kwenye mechi ya jana, Yanga ndiyo ilianza kulifikia lango la Simba dakika ya saba ya mchezo kwa krosi iliyopigwa na Farid Mussa na kuleta kizaazaa kwenye lango, kabla ya kufagiliwa na Mohamed Outtara.

Simba ilijibu dakika moja baadaye, baada ya Clatous Chama kuondoka na mpira kutoka katikati ya uwanja, na kummegea pande Kibu Denis ambaye alipiga shuti, lakini kipa Djigui Diarra alikuwa makini akaudaka mpira huo.



Kibu kwa mara nyingine tena alikosa bao la wazi dakika ya 11, alipounganisha krosi ya Israel Mwenda kutoka winga ya kulia, akiwa anatazamana na kipa Diarra, alipiga nje huku akiwa amezongwa na mabeki wa Yanga.

Hii ni mara ya pili mfululizo kwa Yanga kutwaa Ngao ya Jamii, lakini ikiwa ni mara ya nne kwenye mechi sita ilizocheza dhidi ya Simba.

Mara ya kwanza ilikuwa ni 2001, Yanga ikishinda mabao 2-1, na 2010 Yanga ilitwaa tena kwa kuifunga kwa mikwaju 3-1 ya penalti, baada ya dakika 90 za suluhu, mwaka jana ikiwa ni mara taatu, kabla ya kuchukua tena mwaka huu.

Simba imefanikiwa kutwaa Ngao ya Jamii mara mbili tu mbele ya Yanga, 2011 ikishinda mabao 2-0 na mara ya pili ilikuwa mwaka 2017 kwa mikwaju 5-4 ya penalti.

### SIMBA YAWAHI KUINGIA

Wakati kikosi cha Simba kiliwasili uwanjani saa 11:09 jioni, watani zao Yanga walitia timu dakika 12 baadaye kupitia mlango wa dharula.

Kama ambavyo imekuwa ada pindi timu hizo ziwasilipo kwenye dabi, ndivyo ilivyokuwa muda mfupi kabla ya kikosi hicho cha Wananchi kuwasili. Makomandoo walijipanga kando-kando ya sehemu ambayo gari la timu kubwa lilipotakiwa kupaki kiasi cha kuzua taharuki.

Baadhi ya mashabiki ambao walikuwa wakikatisha eneo hilo, iliwabidi kusogea ili kuona mastaa wao lakini ilikuwa tofauti kwani alionekana kushuka kocha wa timu hiyo, Nasreddine Nabi na viongozi wengine.

Wachezaji hawakuonekana kushuka na tulipofanya utafiti tukabaini kuwa hakuna mchezaji ambaye alikuwepo ndani.

Basi la nyuma ya lile ambalo wengi waliamini lilikuwa na wachezaji ndilo ambalo lilielezwa kuwa lilikuwa na nyota wa kikosi hicho.

Muda mchache baadaye ndipo shangwe lilipoibuka ndani kwani nyota wa Yanga wakiongozwa na Fiston Mayele walikuwa wakiingia kwa mlango usio rasmi (dharula) ambako limekuwa likipaki gari la zimamoto.

Mashabiki wa Yanga walishangilia hadi wachezaji wao walipoingia kwenye vyumba vya kubadilishia nguo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >